# Nipashe

Jumatano Agosti 26, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580320

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## BAKWATA yatoa neno JPM kuchangisha fedha kanisani

UKURASA 5




UKURASA 11

# KUMEKUCHA


**VYAMA** vyalalamikia rafu, madai ya wagombea kutekwa majimboni, Majaliwa, Abood, Hasunga wapita bila kupingwa...*Endelea uk. 2, 3, 4*

## MCHUJO WAGOMBEA URAIS WATIKISA SAA 11, WAWILI WAKATWA

UKURASA 2



Mtamwega Mgaiwa
**SAU**



Twalibul Kadege
**UPDP**



Mtamwega Mgaiwa
**SAU**



Bernard Membe
**ACT-Wazalendo**



John Shibuda
**ADA-TADEA**



Qeen Sendiga
**ADC**



Dk. John Magufuli
**CCM**



Tundu Lissu
**CHADEMA**




Yeremia Maganja
**NCCR Mageuzi**



Hashim Rungwe
**CHAUMA**



Prof. Ibrahim Lipumba
**CUF**



Philipo John Fumbo
**DP**



Leopold Mahona
**NRA**



Khalifan Mazurui
**UMD**



Cesilia Mbaga
**Demokrasia Makini**



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**JPM ATOA MWONGOZO MAGARI YALIYOKAMATWA**
RAIS John Magufuli, jana alikagua magari yaliyodaiwa kuhusika katika matukio ya uhujumu uchumi...

**UKURASA WA 7**

**MTENDAJI MATATANI KWA TUHUMA KUSIMAMIA NYUMBA KUCHOMWA**
OFISA Mtendaji wa Kijiji cha Malangi Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani...

**UKURASA WA 17**

**MWINYI KUCHUKUA FOMU YA URAIS LEO**
MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, kesho anatarajiwa kuchukua...


## MWALIMU KORTINI TUHUMA UBAKAJI

UKURASA 5

**MICHEZO** CARLINHOS AAHIDI MAZITO YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Rais John Magufuli akikagua magari makubwa na madogo 130 yaliyotaifishwa baada ya kuhusika katika matukio mbalimbali ya uhujumu uchumi, yaliyohifadhiwa katika kituo cha mabasi cha zamani, jijini Dodoma jana. Rais aliagiza yagawiwe kwenye taasisi za serikali. **PICHA: IKULU**

# Kumekucha



Kassim Majaliwa



Japhet Hasunga



Abdulaziz Abood

**Na Waandishi Wetu**

KUMEKUCHA! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya kipenga cha kampeni za uchaguzi mkuu kupulizwa rasmi leo, huku baadhi ya wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakikosa upinzani kutokana na kuenguliwa kwa wagombea wa vyama vya upinzani waliojitokeza.

Wagombea wa CCM waliopata bahati hiyo ni pamoja na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye jana alitangazwa kuwa mgombea pekee wa Jimbo la Ruangwa mkoani Lindi aliyekidhi vigezo vilivyowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Vilevile, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alitangazwa kuwa mgombea pekee wa Jimbo la Kongwa mkoani Dodoma baada ya wagombea wa upinzani kudaiwa kutokidhi vigezo vya uteuzi.

Mgombea mwingine wa chama tawala aliyeingia katika kundi hilo ni Abdulaziz Abood, ambaye anatetea ubunge wa Morogoro Mjini. Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Sheila Lukuba, jana alimtangaza Abood kuwa mgombea pekee kutokana na wagombea wengine wa upinzani kudaiwa kufanya makosa katika ujazaji wa fomu za kuomba uteuzi.

Wagombea waliokatwa kwenye jimbo hilo, walitoka Chama cha Wananchi (CUF), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ACT-Wazalendo na CHAUMMA.

Mkoani Songwe, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, amepita bila kupingwa baada ya wagombea kutoka kwa vyama vya upinzani kuenguliwa kwa madai ya kutokidhi vigezo.

Jijini Tanga, Msimamizi wa Jimbo la Tanga Mjini, Daud Mayeji, alitangaza kuenguliwa kwa mgombea ubunge kupitia chama cha ACT-Wazalendo, Rashid Jumbe, kutokana na kile kilichodaiwa kushindwa kuwasilisha picha za utambulisho.

Jijini Arusha, wagombea wa ubunge 14 kati ya 16 katika Jimbo la Arusha Mjini wamepitishwa wakiwamo Mrisho Gambo (CCM) na Godbless Lema (CHADEMA). Waliokatwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo hilo, Dk. John Pima, kutokana na kutokidhi vigezo ni wagombea wa vyama vya ADC na UDM.

Mkoani Kilimanjaro, mgombea wa CUF katika Jimbo la Siha, Baraka Mushi, alienguliwa kutokana na kile kilichodaiwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Ndaki Mhuli kwamba alichelewa.

Pia, mgombea kupitia CHAUMMA katika Jimbo la Mwanga mkoani huko, alienguliwa kutokana na kile kilichoelezwa na Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, kuwa ameshindwa kupata wadhamini 25.

Kampeni za uchaguzi huo zitahitimishwa rasmi Oktoba 27, mwaka huu, siku moja kabla ya uchaguzi wenyewe.

# MCHUJO WAGOMBEA URAIS WATIKISA SAA 11, WAWILI WAKATWA

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imepitisha majina 15 kati ya 17 ya wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya wateule hao kupita katika mchujo uliodumu kwa takribani saa 11 jijini Dodoma jana.

Katika mchujo huo ulioanza majira ya saa 2:35 asubuhi hadi saa moja usiku, Tume iliwaengua wagombea urais wa Chama Cha Kijamii (CCK), David Mwaijolele na mgombea mwenza wake, Ali Saidi Juma, kutokana na kutotimiza masharti ya kikatiba na kisheria.

Vilevile, mgombe wa NLD, Maisha Mchunguzi alienguliwa pamoja na mgombea mwenza wake, kutokana na kutohudhuria uteuzi.

Urejeshaji wa fomu za kuomba kuteuliwa ulifanyika jana katika Ofisi ya NEC jijini, mgombea urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), John Magufuli, na mgombea mwenza wake, Samia Suluhu Hassan, wakifungua pazia la mchujo huo.

Wagombea wengine waliopitishwa baada ya Rais Magufuli ni pamoja na Profesa Ibrahim Lipumba wa CUF, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi), John Shibuda (ADA-Tadea), Muttamwega Mgaywa (SAU), Seif Maalim Seif (AAFP) na Philipo Fumbo (DP).

Wengine ni Leopold Mahona (NRA), Queen Sendiga (ADC), Cecilia Mmanga (Demokrasia Makini), Bernard Membe (ACT-Wazalendo), Hashim Sipunda (CHAUMMA), Twalib Kadege (UPDP), Khalfani Mazrui (UMD) na Tundu Lissu (CHADEMA).

Lissu na mgombea mwenza wake, Salum Mwalimu, ndiyo waliokuwa wa mwisho kuhakikiwa, wakiingia ukumbini majira saa 1:29 usiku na walitangazwa kuteuliwa kuwania nafasi hiyo saa 1:41 usiku.

Kabla ya kuanza kwa uteuzi, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alivitaja vigezo muhimu vilivyozingatiwa kuwa ni pamoja na fomu ya uteuzi kujazwa kikamilifu, wagombea kutoa tamko kwamba wanazo sifa za kugombea, katibu wa chama husika kutoa uthibitisho wa kuwateua wagombea.

Alisema vigezo vingine ni wagombea kudhaminiwa na wapigakura kutoka mikoa 10, wasimamizi wa uchaguzi kuthibitisha majina ya wadhamini, wagombea kutoa tamko mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu kuthibitisha wanazo sifa za kuteuliwa.

### SABABU ZA KUKATWA

Dk. Mahera alitaja sababu za kukatwa kwa wagombea wa CCK kuwa kutowasilisha fomu namba 10 za maadili ya uchaguzi 2020, mbele ya tume zikiwa zimetiwa saini na wagombea wote wawili, yaani mgombea wa chama na mgombea mwenza. Alisema fomu zilizowasilishwa zilikuwa zimetiwa saini ya mgombea urais pekee.

Alisema pia walipaswa kuwasilisha nakala nne za picha za mgombea na mgombea mwenza, lakini zimewasilishwa za mgombea urais tu.

Baada ya kuenguliwa, Mwaijolele alisema ameshindwa kuteuliwa kutokana na kushindwa kufika NEC akiwa na mgombea mwenza kutoka Pemba kutokana na kupatwa na dharura, lakini akaipongeza tume kwa kuzingatia sheria na kanuni.

"Tumekosa fursa hiyo muhimu ingawa tulikuwa na sera nzuri kwa jamii ya Watanzania kwa kuipa kipaumbele sekta ya kilimo. Pamoja na kutopata nafasi hiyo, chama kitashiriki kwenye uchaguzi wa wabunge katika mikoa 16 na madiwani nchi nzima na tutamuunga mkono mgombea ambaye Watanzania watamwona anafaa," alisema.

# CHADEMA walia rafu majimboni

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua hatua za haraka kuhakikisha wagombea wa ubunge na udiwani wa chama hicho katika majimbo manne walionyimwa fomu, wanapata fomu za kuomba uteuzi.

Taarifa ya chama hicho iliyotolewa na Mkuu wake wa Idara ya Habari na Mawasiliano, Tumaini Makene, iliyataja majimbo hayo kuwa Tunduma, Ndanda, Ruangwa na Morogoro Kusini.

"Matendo na matukio hayo siyo tu yanahatarisha amani na usalama, bali pia yanahatarisha mustakabali wa uchaguzi wenyewe," chama hicho kilisema katika taarifa yake hiyo.

Taarifa hiyo ilidai kuwa kwenye Jimbo la Tunduma, mgombea wa udiwani wa Majengo, Boniphace Mwakanjabe, alikamatwa na polisi na kufikishwa mahakamani huku wagombea wengine Moses Mshami (Kata ya Muungano), Florini Mwalongo (Kata ya Maporomoko) na Hosea Kibwana nao wakidaiwa kutafutwa na polisi.

Chama hicho pia kilidai kuwa kwenye Jimbo la Ndanda mkoani Mtwara, mgombea wao wa ubunge wa jimbo hilo, Castor Mmuni, alikamatwa na kushikiliwa na polisi huku kikidai kutishiwa usalama kwa wagombea wake wa ubunge na udiwani katika Jimbo la Ruangwa mkoani Lindi wakidaiwa kutishiwa usalama wao.

Katika Jimbo la Morogoro Kusini, chama hicho kilidai mgombea wa ubunge wa chama hicho, John Mwenegoha, amenyimwa fomu bila kupewa sababu zozote, jambo ambalo ni kinyume cha taratibu.

Alipoulizwa kuhusu malalamiko ya wagombea wa upinzani kunyimwa fomu, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, alisema tume ina taarifa za dosari hiyo na tayari imechukua hatua zinazopaswa.



Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai nchini (DCI), Robert Boaz, akikagua gwaride la askari wa Jeshi la Polisi wilayani Kahama, mkoani Shinyanga jana, akiwa katika ziara ya kikazi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# JPM akagua magari yaliyotaifishwa na kutoa mwongozo wa kuyatumia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, jana alikagua magari yaliyodaiwa kuhusika katika matukio ya uhujumu uchumi na kutaifishwa kisha kuhifadhiwa katika kituo cha zamani cha mabasi jijini Dodoma.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana ilisema baada ya kufanya ukaguzi huo, Rais alitoa maagizo maalum kuhusu matumizi ya vyombo hivyo.

Magari hayo 130, yakiwamo makubwa na madogo, yalikamatwa katika maeneo mbalimbali nchini kisha wahusika kufikishwa mahakamani na mahakama kutoa uamuzi wa kuyataifisha.

Akizungumza baada ya kuyakagua, Rais Magufuli aliipongeza Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Jeshi la Polisi na wote waliohusika kuwakamata waliokuwa wanajihusisha na vitendo hivyo ikiwamo biashara ya meno ya tembo.

Rais, kwa mujibu wa taarifa hiyo, aliagiza magari hayo yagawanywe katika taasisi mbalimbali za serikali ili yatumike kuendesha shughuli za kuwahudumia wananchi na uzalishaji mali.

Taarifa hiyo pia ilieleza kuwa Rais Magufuli aliwapongeza wananchi waliojitokeza kutoa taarifa zilizosaidia kukamatwa kwa watu waliokuwa wanafanya uhalifu kwa kutumia magari hayo.

Sambamba na hilo, Rais aliwaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola ili kukomesha vitendo hivyo.

# Mgombea ubunge CHADEMA kortini madai kuhonga msimamizi

**Na Said Hamdani, LINDI**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Lindi, imemfikisha mahakamani mgombea ubunge Jimbo la Mtama kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Selemani Methew Luwongo (52), kwa madai ya kutaka kumuhonga msimamizi wa uchaguzi.

Methew alifikishwa mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mkoa huo, Maria Batraine na kusomewa shtaka na mwanasheria wa taasisi hiyo, Peter Camilius.

Akimsomea shtaka linalomkabili, mwanasheria huyo wa TAKUKURU, alidai Agosti 24, mwaka huu saa 9 alasiri, mshtakiwa aliyekuwa amechukua fomu ya uteuzi kugombea ubunge wa Jimbo la Mtama mkoani Lindi, alikamatwa akitoa rushwa ya Sh. 1,540,000 kwa msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo.

Mwanasheria huyo alidai kuwa kiasi hicho cha fedha ni kati ya Sh. 10,000,000 anazodaiwa kuzitenga kumpatia msimamizi huyo ili amtangaze mshindi kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Ilidaiwa kuwa kwa kitendo hicho, mshtakiwa amefanya kosa chini ya kifungu cha 15 kifungu kidogo cha (1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana kosa na amepelekwa mahabusu baada ya kutokamilika kwa masharti ya dhamana na shauri hilo namba 83/2020, ambalo litatajwa tena Septemba, 11 mwaka huu.

Wakati mtuhumiwa akipandishwa kwenye karandinga kuelekea Magereza, baadhi ya wanachama, viongozi na wafuasi wa CHADEMA waliokuwa wamekusanyika mahakamani, walionekana kusikitika, huku wakitoa kauli mbalimbali.

**Mwanasheria huyo alidai kuwa kiasi hicho cha fedha ni kati ya Sh. 10,000,000 anazodaiwa kuzitenga kumpatia msimamizi huyo ili amtangaze mshindi kwenye uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.**

# Sugu, Tulia waanza kutambiana

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAGOMBEA ubunge katika Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Akson wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Joseph Mbilinyi 'Sugu' wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamerejesha fomu za kuwania nafasi hiyo, huku kila mmoja akijinasibu kuibuka na ushindi kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Wanasiasa hao walirejesha fomu hizo jana kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Jimbo hilo, Elias Ng'wanidako, kwa nyakati tofauti wakiwa wametofautiana kwa muda wa dakika 50.

Sugu alirejesha saa 4:22 asubuhi na Dk. Tulia akarejesha saa 5:12 asubuhi na kila mmoja aliingia katika ofisi hiyo ya msimamizi wa uchaguzi bila kuwa na mbwembwe za wapambe.

Nipashe ilishuhudia Sugu akiingia katika ofisi za msimamizi kwa kutumia gari dogo aina ya Toyota IST jeusi ambapo alikuwa yeye na jopo la viongozi wanne wa chama hicho wilaya ambao walimsindikiza.

Dk. Tulia aliingia na magari manne ambayo hayakuwa na watu wengi na badala yake moja lilimbeba yeye, lingine liliwabeba wasaidizi wake, lingine liliwabeba viongozi wawili wa CCM Wilaya na gari dogo la Polisi ambalo ilikuwa inaongoza msafara.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhi fomu, Sugu alisema aliamua kwenda kurejesha fomu hiyo kimya kimya kama mbinu mpya ya kufukuzia 'mwizi' kwa maelezo kuwa kila mwaka wanatumia mbinu tofauti.

Alisema muda wa kufanya maandamano na kuwa na kundi kubwa la watu bado haujafika na wataanza baada ya kampeni kuzinduliwa rasmi, ambapo alisema kutakuwa na maandamano na nyimbo za kutosha.

"Muda wa mtiti (mkusanyiko wa watu) tutaanza Septemba 5 ambapo mgombea urais wetu Tundu Lissu, atakuwapo hapa. Sasa leo (jana) tumeona tuje kimya kimya na si kama tulivyofanya wakati wa kuchukua fomu na tuna uhakika tutashinda," alisema Sugu.

Dk. Tulia alisema baada ya kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi hiyo ya ubunge, ana uhakika yeye pamoja na chama chake cha CCM wataibuka na ushindi.

Alisema amejiandaa vizuri kuhakikisha anashinda kwenye uchaguzi huo na kwamba anapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa wanachama wengine na viongozi wa CCM.

"Tuna uhakika vyama vyote vimejipanga vizuri, lakini sisi CCM tumejipanga vizuri zaidi na nina uhakika tutashinda na kulirejesha jimbo hili ndani ya chama chetu," alisema Dk. Tulia.

Jimbo la Mbeya Mjini kwa miaka 10 kuanzia 2010, lilikuwa linaongozwa na CHADEMA chini ya Sugu ambaye katika uchaguzi wa mwaka huu anakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Dk. Tulia.



Vibarua wakichanganya zege kwa ajili ya ujenzi unaoendelea wa uzio wa eneo la machinjio mpya ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbaroni madai ya kumteka mgombea udiwani CHADEMA

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MTU mmoja (jina linahifadhiwa) anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Pwani kwa tuhuma za kuhusika kumteka nyara mgombea udiwani kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kata ya Kerege Wilaya ya Bagamoyo, Martine Sultan.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 22, mwaka huu, katka Kitongoji cha Manofu, Kerege ambapo watu wanne wanaodaiwa kuwa wanaume, walimteka mgombea huyo.

Wankyo alisema baada ya jeshi hilo kupata taarifa, walifuatilia na kumkamata mmoja wa watuhumiwa hao akiwa katika Kijiji cha Janga, Mlandizi wilayani Kibaha.

Alisema mtuhumiwa huyo pamoja na mgombea udiwani, walikutwa katika eneo hilo wakitumia gari aina ya Toyota RAV4 (namba zimehifadhiwa).

Kwa mujibu wa Kamanda Wankyo, chanzo cha tukio hilo bado hakijafahamika na kwamba watu wengine watatu bado hawajajulikana walipo.

Kamanda Nyigesa alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea ikiwa ni pamoja na kuwakamata watuhumuwa wengine watatu. aliomba mwananchi yeyote mwenye taarifa kuhusiana na tukio hilo, atoe ushirikiano kwa njia yoyote na vyombo vya dola.

Katika tukio lingine, Jeshi la Polisi linamshikilia Gale Salabo (32) mkazi wa Mafumbi wilayani Kisarawe kwa tuhuma za kumuua babu yake, Haima Nasri.

Kamanda Nyigesa alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11:00 jioni katika eneo la Mafumbi.

Alisema taarifa za awali zinadai kuwa mtuhumiwa alifanya mauaji hayo baada ya kumtuhumu marehemu kuiba 'sola panel' yake.

Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Kituo Cha Afya Chole na mtuhumiwa anashikiliwa kwa mahojiano na upelelezi ukikamilika, atafikishwa mahakamani.

# Mgombea wa ubunge avamiwa, aporwa fomu

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

MGOMBEA ubunge wa Morogoro Mjini kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Abeid Mlapakolo, amelishukuru Jeshi la Polisi Mkoa wa Morogoro kwa kufanikisha kupatikana kwa fomu zake za kugombea ubunge wa jimbo hilo zilizokuwa zimeporwa na watu wasiojulikana.

Mlapakolo alisema tukio la kuvamiwa na kuporwa fomu hizo lilitokea jana asubuhi wakati akienda kwenye ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo kutekeleza matakwa ya sheria za uchaguzi kurejesha fomu kabla ya saa 10.

Alidai kuwa, akiwa nje ya jengo la ofisi ya msimamizi wa uchaguzi, ghafla kulitokea kundi la watu waliomvamia na kuanza kumshambulia kwa kumpiga sehemu mbalimbali za mwili kisha kumpora fomu na kutokomea nazo.

"Nilifika kurejesha fomu kama sheria inavyotaka kila mgombea arejeshe fomu kabla ya saa 10 jioni, lakini nikiwa nje, likaja kundi la watu kunivamia na kunipiga, wengine wakataka kunivunja mkono na fomu zangu wakakimbia nazo.

"Ninamshukuru Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, nilipompigia simu alinisaidia wale watu walikamatwa na fomu zangu zikarudi," alisema Mlapakolo.

Aliliomba jeshi hilo kuimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali kuelekea uchaguzi mkuu kufuatia vitendo vya uvunjifu wa amani vinavyoendelea hasa kuvamiwa kwa baadhi ya wagombea wa upinzani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo ambapo watuhumiwa wa tukio hilo wameshakamatwa na wanaendelea kuhojiwa.

Aliwataka wananchama wa chama hicho kuwatulivu wakati hatua za kisheria zinaendelea kuchukuliwa na kwamba uchunguzi utakapokamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani.

**"Nilifika kurejesha fomu kama sheria inavyotaka kila mgombea arejeshe fomu kabla ya saa 10 jioni, lakini nikiwa nje, likaja kundi la watu kunivamia na kunipiga, wengine wakataka kunivunja mkono na fomu zangu wakakimbia nazo.**

HABARI KITAIFA

# BAKWATA yatoa neno JPM kuchangisha fedha kanisani

**Na Romana Mallya**

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), limetoa msimamo wake kuhusu Rais John Magufuli kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa msikiti akiwa kanisani, likieleza kuwa kitendo hicho ni cha uzalendo, upendo na uungwana.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Rais Magufuli alianzisha harambee ya ujenzi wa msikiti wakati wa ibada ya uzinduzi wa Parokia ya Bikira Maria Emmaculata ya Kanisa Katoliki Parokia jijini Dodoma.

Katika harambee hiyo, Rais Magufuli alifanikiwa kuchangisha Sh. milioni 48.21, mifuko 48 ya saruji na malori matano ya mchanga.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu wa Baraza la Ulamaa, BAKWATA, Sheikh Hassan Chizenga, kwa niaba ya Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, alisema baada ya harambee hiyo, kulitokea mawazo msigano kuhusu wakristo kuchangia ujenzi wa msikiti.

"Baadhi ya watoa mawazo wakitumia nafasi hii kumkashifu Rais wetu, wengine wakitia shaka kuhusu uhalali wa jambo hili katika misingi ya dini ya kiislamu," alisema.

Alibainisha kuwa Mufti Mkuu Sheikh Zubeir ameweka bayana msimamo wa BAKWATA kwenye jambo hilo kuwa kilichofanywa na Rais Magufuli ni kitendo cha uzalendo, upendo na uungwana kilichohuisha moyo wa mshikamano baina ya waumini wa kiislamu na wakristo.

"Ni jambo ambalo lilikuwapo tangu zama za Mtume (SAW) na Mungu mwenyewe kalisifia. Amesema Mungu katika Quran Surati Maaida Aya ya 82.

"Na utakuta wakaribu zaidi kimapenzi kwa wale walioamini (yaani Waislam) ni wale waliosema sisi ni Manaswara (yaani Wakristo) hii ni kwa kuwa miongoni mwao wamo makasisi na Mapadre na kuwa wao hawana kiburi," alinukuu Sheikh Chizenga.

Alisema kitendo alichokifanya Rais Magufuli kinahuisha uhalisia wa maneno ya Mungu na kwamba ni kizuri na kinachostahiki kushukuriwa na kupongezwa.

"Ninachukua nafasi hii kumshukuru Rais Magufuli na Baba Askofu aliyeruhusu hili kufanyika kanisani kwake. Ninavitaka vyombo vya habari kutousemea Uislamu kwa kuuzulia na watambue Msemaji Mkuu wa Waislamu ni BAKWATA," alisema.

Kuhusu fedha hizo, Mufti Mkuu Sheikh Zubeir alisema uchambuzi wa kina wa maulamaa wa dini ya Kiislamu wanatambua fedha zile ni halali kutumika kujengea msikiti bila ya shaka.

"Maulamaa wametoa Fatwa hii kwa kutegemea mashiko mengi, miongoni mwa hayo ni kule Mtume kukubali kupokea zawadi mbalimbali kutoka kwa viongozi wa dini ya kikristo kama vile Kaizari na Mukaukasi na kutoka kwa Mfalme wa Misri kabla ya kuingia katika Uislamu na wanasema.

"Pale inapojuzu kupokea zawadi kwa asiyekuwa Muislamu kumiliki na kuitumia, basi hapana ubaya kuijengea Msikiti au kuitumia mali hiyo katika lolote lenye maslahi kwa Waislamu," alisema.

Katika hatua nyingine, Mufti Mkuu Sheikh Zubeir amewaomba Watanzania kufunga siku tatu kuiombea Tanzania ivuke salama katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, ukitanguliwa na kampeni za wagombea zinazoanza leo na kuhitimishwa Oktoba 27.

"Tarehe ya kufunga itaanzia Agosti 29 hadi Agosti 31 ikiwa ni sawa na mwezi 9-10-11 za Maharram 1442 Hijiriyya, katika siku hizi Watanzania wenye uwezo wa kufunga wafunge kwa lengo la kumkabidhi Mungu nchi, avishike yeye na mioyo yetu aichague yeye na hatma ya nchi iwe mikononi mwake Mungu," alisema.

Alisema wamechagua siku hizo kwa kuwa zilitukuzwa tangu zama za Mtume Musa (AS) hadi zama za Mtume Muhammad (SAW) kwa kuwa ndizo waliyookolewa Mtume Musa na wana Israel wakavuka bahari bila chombo.

Aliwakumbusha Watanzania kuwa wameokolewa kwenye janga la corona kwa maombi na wasikubali kukaa mbali na silaha hiyo ya maombi.



Msemaji wa Mufti wa Tanzania, Sheikh Hassan Chezenga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, akiwataka Watanzania kufunga siku tatu kuiombea nchi ivuke salama katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwalimu kortini tuhuma za kumbaka mwanafunzi

**Na Welingtone Masele, IGUNGA**

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Nanga, Keby Aaron (32), amefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa kidato cha tatu (jina linahifadhiwa) mwenye umri wa miaka 17.

Mwendesha Mashtaka wa Polisi Wilaya ya Igunga, Elmajid Kweyamba, aliiambia mahakama mbele ya Hakimu Mkazi Lydia Ilunda kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo kinyume na kifungu 130 (1) (2) (e) (1) cha Kanuni ya Adhabu sura ya 16 mapitio ya 2019 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Alidai kuwa mtuhumiwa alifanya mapenzi na mwanafunzi huyo Machi na Mei, mwaka huu kwa nyakati tofauti majira ya usiku katika maeneo ya shule huku akijua kufanya hivyo ni kosa.

Baada ya kusomewa shtaka hilo, mtuhumiwa alikana kutenda kosa hilo na yuko nje kwa dhamana ya Sh. milioni moja.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Septemba 30, mwaka huu, itakapoanza kusikilizwa.

Mwendesha mashtaka aliiambia mahakama kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

## Watatu washikiliwa madai udanganyifu

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kufanya udanganyifu kwa kutengeneza barua bandia ya utambulisho kutoka Chama cha Sauti ya Umma (SAU) na kutaka kuchukua fomu ya kugombea ubunge Jimbo la Morogoro Mjini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbrod Mutafungwa, alisema jeshi hilo lilipokea taarifa kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo hilo, Sheila Lukuba, akitilia shaka barua ya utambulisho kutoka kwa Edga Msigwa akidai kuwa ni mwanachama wa SAU.

"Tulipopata taarifa ya kutilia shaka kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi, tulifika ofisini kwake na tulipokagua hiyo barua tulikuta ina mapungufu na hata tulipochunguza tumebaini chama cha SAU hakina hata ofisi ya wilaya au mkoa ndani ya Morogoro," alisema Mutafungwa.

Alisema baada ya kumhoji alikiri kuwa si mwanachama wa chama hicho bali alipewa barua hiyo na Christian Daniel ambaye ni mratibu wa uchaguzi wa madiwani wa manispaa ya Morogoro pamoja na dereva wa mgombea ubunge Jimbo la Morogoro Mjini kupitia CHADEMA aliyetambulika kwa jina moja la David.

Kamanda Mtagungwa alisema watuhumiwa wote watatu wanaendelea kuhojiwa ili kujua sababu zilizopelekea kufanya udanganyifu huo.

"Tunamshikiria huyu ni dereva wa Devotha Minja, mgombea kupitia CHADEMA, ndiye alitumia gari ya mbunge huyo kumbeba Edga Msigwa, ambaye alikuwa na barua ya kughushi kwa hiyo tumemkamata yeye pamoja na gari alilolitumia," alisema Mutafungwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wizara ya Mifugo inastahili pongezi kwa mageuzi haya

MWISHONI mwa wiki iliyopita, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilibainisha mafanikio ya utendaji wake kwa miaka mitano ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano.

Taarifa iliyotolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kuhusu utendaji hao, ilionyesha kuwa na mageuzi makubwa kwenye sekta zote mbili zilizo chini ya wizara hiyo kwa maana ya mifugo na uvuvi.

Katika taarifa yake hiyo, Waziri Mpina alisema kuwa kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka huu, idadi ya mifugo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, akibainisha kuwa idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 25.8 hadi milioni 33.4, mbuzi milioni 17.1 hadi milioni 21.29, kondoo milioni 4.8 hadi milioni 5.65 na kuku milioni 37 hadi milioni 83.28.

Vilevile, alisema uzalishaji wa maziwa nao umeongezeka kutoka lita bilioni 2.1 mwaka 2015/2016 hadi kufikia lita bilioni tatu mwaka 2019/20 wakati uzalishaji wa nyama nao umeongezeka kutoka tani 636,559 mwaka 2015/2016 hadi tani 701,679.1 mwaka 2019/20.

Waziri Mpina alisema kuwa katika kipindi hicho, serikali pia ilitunga na kuzifanyia marekebisho sheria na kanuni zilizopitwa na wakati zilizobainika kusababisha usumbufu kwa wananchi.

Alibainisha kuwa sheria na kanuni zilizofanyiwa marekebisho katika sekta ya mifugo ni 27 ikiwamo kutungwa kwa kanuni mpya ya uogeshaji mifugo na utoaji wa chanjo.

Waziri huyo pia alisema serikali imefanikiwa kudhibiti utoroshaji na udanganyifu katika biashara ya ngozi kwa kutoza asilimia 80 ya usafirishaji wa ngozi ghafi na asilimia 10 ya usafirishaji wa ngozi zilizosindikwa kufikia hatua ya kati.

Sambamba na hayo, Mpina alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano, serikali imejenga kiwanda kipya chenye uwezo wa kuzalisha jozi na soli za viatu 1,200,000 kwa mwaka, kuchakata ngozi futi za mraba 13,000,000 kwa mwaka na kuzalisha bidhaa mbalimbali za ngozi.

Kwenye sekta ya uvuvi, Waziri Mpina alisema serikali imefanikiwa kufanya mapitio na kuboresho ya sheria, kanuni, mipango na tozo mbalimbali zinazosimamia sekta ya uvuvi, ili ziwe rafiki kwa watumiaji na hivyo kupunguza vitendo vya ukiukwaji wa sheria na kanuni za uvuvi kwa uendelevu wa rasilimali za uvuvi.

Aliyataja mafanikio mengine katika sekta hiyo kuwa ni ujenzi wa bandari ya uvuvi, kuanza kwa uvuvi katika bahari kuu, uzalishaji wa mazao ya uvuvi kwenye maji ya asili, usindikaji na usafirishaji wa minofu ya samaki na mazao mengine ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na uzalishaji wa samaki katika mabwawa na vizimba.

Nipashe tunaipongeza wizara hiyo ya mageuzi hayo makubwa yaliyoifanya iwe na mchango mkubwa kwa uchumi wa nchini, sekta ya mifugo yenye ukuaji wa asilimia tano (mwaka 2019) ikichangia asilimia 7.4 ya Pato la Taifa, huku sekta ya uvuvi inayokua kwa asilimia 9.2, ikichangia asilimia 1.71 ya pato la taifa.

Tunaamini mafanikio haya yamechagizwa na kuwapo kwa mikakati ya kuongeza uzalishaji katika sekta hizo mbili kulikokwenda sanjari na udhibiti wa biashara ya mifugo na uvuvi pamoja na mazao yake.


Nipashe tunaikumbusha wizara kuendelea kushughulikia dosari kadhaa zilizojitokeza katika utendaji wa sekta za mifugo na uvuvi, hasa kuwekeza zaidi kwenye uvuvi wa bahari kuu ambao nchi bado iko nyuma katika kutumia fursa ya eneo kubwa la bahari ililonalo.

Kuna baadhi ya mataifa ambayo yameweza kupaa kiuchumi kwa kutegemea rasilimali ya bahari tu (blue economy), hivyo serikali hainabudi kuliwekea mkazo eneo hili.

Tunaishauri serikali kuwekeza zaidi katika sekta za mifugo na uvuvi kupitia uzalishaji wa wataalamu na utafiti ili zichangie kikamilifu katika pato la taifa, ikizingatiwa kuwa nchi yetu inashika nafasi ya pili Afrika kuwa kuwa na mifugo mingi pamoja na bahari, maziwa na mito lukuki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Siasa ndiyo maisha wananchi wasiikwepe

NENO siasa limekuwa likitafsiriwa kwa maana nyingi, zikiwamo zile ambazo zinawafanya baadhi ya watu kuichukulia tofauti na kujiweka pembeni kana kwamba haina maana katika maisha yao.

Wapo wanaoamini kwamba, siasa ni mchezo mchafu na wengine wanasema, wanasiasa ni waongo, hivyo hawataki kuwasikiliza wala kujihusisha nao kwani hakuna lolote jipya.

Kutokana na tafsiri hizo, baadhi hawataki kushiriki katika uchaguzi ili kupiga kura ama kuchaguliwa, badala yake hujiweka pembeni na kuwa watazamaji wa kile kinachoendelea katika siasa.

Lakini, kama kamusi ya Kiswahili sanifu, inavyoelezea maana mbili ya neno siasa, ikisema ni itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya wahusika.

Maana ya pili ya neno siasa iliyopo katika kamusi hiyo inaelezea kuwa ni mbinu ya utekelezaji au uendeshaji wa jambo kwa kutumia busara na hekima ili kufikia lengo linalotarajiwa.

Kwa upande wa wachambuzi wa siasa nao hawako nyuma wanaieleza kuwa ni utekelezaji wote wa mkataba kati ya watawala na watawaliwa, msingi wake ukiwa ni katiba na demokrasia, ambayo ni serikali ya watu, inayoongozwa na watu kwa manufaa ya watu.

Yawezekana neno siasa lisiewe na maana ya moja kwa moja kwamba ndiyo halisi, lakini maana hizo na nyingine nyingi, inaelezea jinsi, ambavyo watu wanavyohusika katika siasa kwa ajili ya manufaa yao.

Kwa ujumla ni kwamba, siasa ni maisha na haikwepeki ingawa kumekuwapo na misemo mbalimbali, ukiwamo wa 'siasa ni mchezo mchafu', hali ambayo inasababisha baadhi ya Watanzania kujiona hawahusiki katika siasa.

Jambo muhimu kutambua ni kwamba, viongozi wote kuanzia chini kwenye serikali za mitaa hadi rais, hutokana na siasa, na ndiyo huamua masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya watu.

Hivyo, Watanzania waliozoea kusema kwamba; 'mimi siyo mwanasiasa sitaki siasa', na kujiweka pembeni wakati wa uchaguzi, wajue siasa inatawala maisha yao, na hawana pa kuikwepea.

Ni vyema wakatambua kuwa kila Mtanzania anahitaji ulinzi na kuishi kwa amani, afya, elimu na mambo mengi ya msingi katika nchi yake, wenye jukumu la kuwahakikisha hayo ni viongozi wanaotokana na siasa.

Kutokana na majukumu yao, ndiyo maana vyama huandaa kila mwaka wa uchaguzi, kutayarisha ilani zinazoelea mambo mbalimbali ya maendeleo ambayo vinapanga kuyafanya vikipewa ridhaa na wananchi.

Kwa hiyo, wale ambao wanaishi kwa mazoea wakiamini kwamba, siasa haiwahusu, ni vyema wakaachana na mazoea hayo na kama wameajiandikisha katika daftari za kudumu la wapigakura, basi washiriki uchaguzi mkuu.

Iwapo hawajawahi kujiandikisha katika daftari hilo, basi miaka mingine wajiandikishe ili wachague viongozi wanaowataka, kuliko kuendelea kujiweka pembeni na kuachia wengine wawachagulie.

Kwa mtindo huo wa kujiweka pembeni, yawezekana wamechangia kuwapo kwa viongozi wasiofaa katika maeneo yao, kwa kuwa kuwapo ama kukosekana kwa kura moja inaweza kubadilisha matokeo ya uchaguzi.

Maana yangu ni kwamba, inawezekana akiwapo mgombea ambaye wapigakura hawamtaki, na njia pekee ni kuchagua mwingine, siyo kubaki nyumbani na kuamini atakosa kura, wengine watamchagua.

Pamoja na hayo, kila Mtanzania akitambua kuwa siasa ni maisha, hakutakuwapo na kisingizio cha kujiweka pembeni, badala yake wote watashiriki katika uchaguzi wa viongozi katika uchaguzi mkuu.

Leo kipenga cha kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu kitapulizwa kwa ajili ya wagombea urais, ubunge na udiwani kunadi ilani na sera za vyama vyao, hivyo ni nafasi kwa wapigakura kwenda kuwasikiliza.

Wakati mwingine inawezekana watu wanachukia siasa labda kutokana na baadhi ya watu wanaochaguliwa kuusaliti umma kwa kwenda kinyume na yale waliotarajia na hivyo kusababisha wakate tamaa kupigakura.

Lakini, njia pekee ya kuachana na viongozi wa aina hiyo, ni kujitokeza kwa wingi na kuwapigia kura wengine, badala ya kujiweka pembeni na kulalamika.

# Mtendaji matatani kwa tuhuma kusimamia nyumba kuchomwa

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

OFISA Mtendaji wa Kijiji cha Malangi Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, ameingia matatani baada ya mkazi mmoja wa eneo hilo kumshtaki kwa Mkuu wa Mkoa huo, Joseph Mkirikiti, kuongoza watu kuimwagia nyumba yake petroli na kisha kuiteketeza kwa moto.

Inadaiwa kwamba watu waliofanya kitendo hicho walikuwa wamevaa ngozi nyeupe.

Jana, mkazi huyo Cecilia Baria, aliangua kilio mbele ya Mkirikiti, alipofika kijijini hapo kuzungumza na wananchi, ambapo alimweleza kuwa tukio hilo limesababisha yeye na familia yake kuishi chini ya mti kwa miezi sita sasa.

Kutokana na malalamiko hayo, Mkirikiti alimwagiza Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi, Paul Kasabago na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, kuchunguza sakata hilo na kumpa majibu kabla ya Agosti 30, mwaka huu.

Akieleza mkasa huo, Baria alisema makazi yake yalichomwa moto na watu hao bila yeye kuwapo, lakini alipofika nyumbani alielezwa na wanawe kwamba mtendaji huyo alifika hapo akiwa na watu wenye ngozi nyeupe na kuimwagia nyumba yao petroli.

"Halafu pia nilipofika nilikuta watoto wangu wamechapwa viboko na watu hao waliokuwa na mtendaji pamoja na mwekezaji anayeishi katika kijiji hicho," alieleza na kuendelea:

"Nguo zangu zote ziko ofisini, chakula na vitu vyangu vyote vinashikiliwa na kila ofisi niliyoenda kuomba msaada sijasaidiwa, mimi na wanangu tunaishi chini ya mti."

Alipoulizwa kuhusiana na malalamiko hayo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Maisaka, Catherine Koila, alisema nyumba ya mama huyo ilivunjwa na Mtendaji wa Kijiji cha Malangi kwa amri ya Mahakama.

Kwa mujibu wa Koila, Mahakama ilijiridhisha kwamba mume wa mama huyo alivamia eneo la mwekezaji akitokea Kijiji cha Imbilili, Kata ya Sigino. Koila alisema tangu nyumba hiyo kuvunjiwa imepita takribani miezi sita au saba baada ya kutolewa kwa amri ya mahakama mwaka jana.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu huyo wa mkoa alieleza kushangazwa kwake na tukio hilo, huku akihoji iweje viongozi wote wa eneo hilo washindwe kumsaidia mama huyo hata kujengewa nyumba nyingine, baada ya mkasa huo.

Aidha, baada ya kusikiliza utitiri wa kero za wananchi ambapo asilimia 97 ya kero zilizoibuliwa zilikuwa za ardhi, alisema atazimaliza hata kama zingekuwa 2,000 angezipatia ufumbuzi wa kudumu.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo kutafuta ufumbuzi wake ndani ya siku saba, na akishindwa amsukumie na yeye na hata yeye akishindwa, atazipeleka kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi.



Mkuu wa Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, Abbas Kayanda (kushoto), akikagua jengo la choo cha mnadani wilayani humo jana, linalojengwa baada ya kutelekezwa kwa muda mrefu. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Madereva magari ya kemikali waipa neno serikali, wananchi

**Na Mary Geofrey**

MADEREVA wanaondesha magari yanayosafirisha kemikali nchini, wameiomba serikali kutoa elimu kwa jamii inayoishi pembezoni mwa barabara ili kuepuka madhara yatokanayo na ajali za kemikali.

Walitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam jana kupitia kwa mwakilishi wao kutoka Kampuni ya Ramada Transport, Abdulrazak Omar, wakati wa kufunga mafunzo ya siku mbili ya madereva 99 wanaoendesha magari yanayosafirisha kemikali iliyotolewa na Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

Alisema licha ya kupewa mafunzo hayo, bado elimu inahitaji kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa barabara ili kuepuka madhara kama ilivyotokea kwa ajali ya kuanguka kwa lori la mafuta mkoani Morogoro Agosti mwaka jana na kusababisha vifo vya watu takribani 70.

"Tunashukuru kwa mafunzo tuliyopatiwa siku ya leo (jana), tunaamini yatakuwa msaada mkubwa kwetu. Lakini bado tuna ombi kwa serikali, watoe elimu hii pia kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa barabara ambazo tunapita.

"Sisi tuna elimu ya kujikinga na kuepusha madhara yatokanayo na ajali za kemikali, lakini wananchi wao bado hawana elimu ndiyo sababu ajali ikitokea wanakimbilia eneo la hatari kuanza kufungua vitu," alisema Omar.

Kaimu Mkemia Mkuu wa Serikali, Sabanitho Mtenga, akifunga mafunzo hayo kwa niaba ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fedelice Mafumiko, alisema kupitia elimu wanayotoa, kunasaidia kuwa na madereva wenye weledi wa usafirishaji salama wa kemikali.

"Matarajio yangu ni kuwa baada ya mafunzo haya, mtazingatia taratibu za usafirishaji salama wa kemikali kwa mujibu wa sheria na kanuni zake za mwaka 2015 katika nyanja zote," alisema Mtenga.

Aliwataka madereva hao kuwa mabalozi wazuri wa kuhamasisha wadau na madereva wengi zaidi kupata mafunzo hayo pamoja na kueneza elimu hiyo katika maeneo yao ya kazi, ili kulinda afya za watu na mazingira.

Katika mafunzo hayo, madereva hao walifundishwa kuhusu Sheria za Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Majumbani ya Mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2015, usafirishaji salama wa kemikali, madhara ya kemikali kwa afya na mazingira, ajali za kemikali na wajibu wa madereva wanaosafirisha kemikali.

## Vijana wasisitizwa kudumisha amani

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

VIJANA kisiwani Pemba wametakiwa kusimamia na kudumisha amani iliyopo nchini hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka.

Akizungumza na vijana katika kongamano la amani na utulivu kwa vijana lililofanyika katika Uwanja wa Michezo Gombani Chake Chake, Naibu Mufti Zanzibar, Sheikh Mahmoud Mussa Wadi, alisema, historia ya amani ilianza tangu mwanzo wa dunia hivyo ni vyema kuiendeleza.

Alisema kipindi cha uchaguzi ni kigumu sana, hivyo ipo haja kwa vijana kuiendeleza amani iliyopo na kuisimamia kwani pasi na amani hakuna furaha wala maendeleo.

"Kipindi tunachoelekea ni kigumu sana, hivyo tutakapoivunja amani yetu, itasababisha maendeleo yote ya miaka mitano yatavunjwa kwa siku moja, tuwe makini", alisema Naibu Mufti.

Alieleza vijana ni watu muhimu katika kusimamia na kuimarisha amani, na ndio maana wakaanza kuwaelimisha wao, kwani yanayosemwa katika jamii huamsha hisia za watu, na ndipo amani inapoweza kuvunjwa.

Sheikh Wadi alisema kuwa amani ni jambo muhimu sana katika nchi na kuitaka jamii izingatie umuhimu wake kwa kuwa ni mafunzdisho kutoka kwa Mtume Muhammad (S.A.W) na imeshazungumzwa katika Qur-an tukufu.

Akiwasilisha mada ya amani na utulivu katika misingi na mtazamo wa kiislamu, Sheikh Said Ahmad Mohamed, alisema hakuna maendeleo pasi na kuwApo amani.

Nae Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Chake Chake Mfaume, Mussa Mohamed, katika mada yake kuhusu amani na utulivu kwa misingi ya sheria, taratibu, kanuni za nchi, alisema viashiria vya uvunjifu wa amani ni vingi sana hasa katika kipindi cha kuelekea uchaguzi, hivyo wachukue juhudi ya kuelimisha jamii.

Mchungaji Benjamin Kisanga wa Kanisa la Aglikana Vitongoji, alishukuru sana kuandaliwa kongamano hilo kwa vijana na kusema amani ni kwa watu wote, hivyo iwapo itaisimamiwa ipasavyo kwa pamoja itaidumishwa.

Imamu wa Msikiti Vitongoji Chake Chake, Abdalla Mohamed Abdallah, alisema suala la amani limezingatiwa katika uislamu, hivyo idumishwe.

Askofu wa Anglikana Zanzibar, Michael Hafidh, aliwataka vijana kutoingia katika kipindi cha mkwamo kwani wao ni watu muhimu sana na amani ndio inayowaweka watu pamoja.

Mapema Meneja Mradi wa kutafuta kundi maalumu kwa ajili ya amani, Jamaly Ally Hussein, alisema lengo lao ni kukutana, kuwajengea uwezo vijana na kuwawezesha katika suala la amani, ili iweze kudumu.

# TNBC: Wawezeshe vijana washiriki ujenzi wa uchumi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Godwill Wanga, amewaomba wawekezaji na wafanyabiashara kuwahusisha kwa vitendo vijana katika miradi itakayowawezesha kujiajiri na kuchangia ujenzi wa uchumi wa taifa.

Akizungumza katika ofisi za Kampuni ya Agricom Africa, tawi la Igurusi mkoani Mbeya Dk. Wanga, aliipongeza kampuni hiyo kwa kutoa ajira kwa vijana wa Igurusi wanaotengeneza matrela ya kuunganishwa kwenye pawatila na matrekta.

"Nimefurahishwa namna kampuni hii inavyotekeleza dhana ya ushirikishaji. Kampuni hii imetoa ajira kwa vijana wa Igurisi kutengeneza matrela ya kuunganisha kwenye pawatila na matrekta. Hatua hii siyo tu inatoa ajira kwa vijana bali pia inakuza uchumi wa ndani ya nchi," alisema Dk. Wanga.

"Naomba kampuni nyingine nchini ziige mfano wa Agricom kwa kuwashirikisha vijana katika miradi mbali mbali. Hatua za aina hiyo zitachochea maendeleo na nchi itapiga hatua kiuchumi," aliongeza Dk. Wanga.

"Nimekuja kujioena namna kampuni hii inavyofanya kazi ya kusambaza zana za kilimo kwa wakulima nchini. Usambazaji wa zana unaimarisha uzalishaji wa mazao na kuchochea ujenzi wa viwanda na nimeona ushirikishwaji wa wananchi unavyofanywa na kampuni hii," alieleza Dk.Wanga

Dk Wanga amewaomba vijana na wanawake kukuza ubunifu wa biashara na uthubutu ili waweze kunufaika na Sh. bilioni 20 ambazo Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) limekabidhiwa na serikali ili kuwakopesha vijana na wanawake ili kukuza biashara zao.

Fundi wa matrela wa Igurusi, Shukuru Msongole, aliishukuru Kampuni ya Agricom Africa kwa kuwapa zabuni ya kuunda matrela ya pawatila na matrekta zaidi ya 100 na ameahidi kuifanya kazi vizuri na kwa wakati.

Mmiliki wa Agricom Africa, Angelina Ngalula, alisema kampuni yao inahitaji matrela 300 za pawatila Igurusi. Alisema zaidi ya Sh. milioni 700 zitatolewa kwa wazalishaji wa matrela na kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo.



Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa (wa tatu kulia), akikata utepe kuzindua tawi la benki ya NMB Mlimba wilayani Kilombero, mkoani Morogoro jana. Kushoto ni Meneja wa benki hiyo, Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus, Meneja wa tawi la NMB Mlimba, Omary Mtibiro na Kaimu Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Salie Mlay. Habari Uk. 9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TADB yahamasisha ufugaji ng'ombe wa maziwa

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imehamasisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kukabiliana na upungufu wa bidhaa hiyo katika kiwanda cha kuchakata maziwa cha jijini Tanga.

Kiwanda hicho kinakabiliwa na upungufu wa maziwa kutoka kwa wafugaji.

Hayo yalibainishwa na Mtendaji Mkuu wa kiwanda hicho, Innocent Mushi jana alipokuwa akitoa maelezo kwa ujumbe wa TADB ulioongozwa na na Mkurugenzi Mtendaji, Japhet Justine.

Hata hivyo, Mushi aliishukuru TADB kwa kuiwezesha kujenga miundombinu ya kisasa ya kupokea maziwa inayokiwezesha kupokea maziwa yakiwa safi na salama.

"Tumejenga vituo vya kisasa ili kurahisisha ukusanyaji wa maziwa kutoka kwa wafugaji wa maeneo mbalimbali katika jiji la Tanga. Miundombinu hii inasaidia kupunguza upotevu wa maziwa au kuharibika njiani kwani wengi wafugaji wanatoka maeneo ya mbali na kiwanda kilipo," alieleza Mushi.

Alisema Tanga Fresh imenufaisha zaidi ya wafugaji 6,000 kwa kununua maziwa yao katika maeneo mbalimbali mkoani Tanga na mikoa ya jirani ya Kilimanjaro na Arusha na pia mikoa mingine ya Morogoro, Mbeya na Njombe.

Justine aliuomba Mkoa wa Tanga kuongeza idadi ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa sababu Tanga Fresh ni soko kubwa la maziwa kwa wafugaji wa Mkoa wa Tanga na mikoa mingine.

"TADB imekopesha vyama viwili vya ushirika ya wafugaji na vinasambaza maziwa kwa wananchi na kukiuzia maziwa Tanga Fresh. Tumo mbioni kuviwesesha vyama 26 ili kuboresha mnyororo wa thamani wa malighafi hii na kuinua mapato ya wafugaji mkoani humu," alisema Justine.

Aliwaomba wafugaji kuunda vyama vya msingi vya ushirika ili waweze kupata mikopo ya masharti nafuu kutoka TADB na benki za CRDB, NMB, StanicBank.

Bw Justine alisifia ujenzi wa vituo vya kupokea maziwa Jijini Tanga na kusema miundombinu hiyo ni hatua muhimu katika kuinua mnyoyoro wa thamani wa malighafi ya kiwanda hicho.

"Ujenzi wa vituo hivi utasaidia upatikanaji wa malighafi hiyo kwa urahisi na kwa ubora unaotakiwa ili hata bidhaa zitakazozalishwa ziwe na bora unaotakiwa sokoni," alisema.

Alisema viwanda vya maziwa vya Tanzania vina uwezo kuwa kuchakata lita 150,000 za maziwa kwa siku, lakini havipati maziwa ya kutosha.

# CUF yateua 136 kuwania ubunge

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimetangaza majina ya wagombea wake 136 kiliowateua kuwania ubunge katika majimbo ya Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa taarifa ya chama hicho iliyotolewa jana na kwa vyombo vya habari, miongoni mwa wateule hao ni Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Tanzania Bara, Magdalena Sakaya (Kaliua), na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara, Maftaha Nachuma (Mtwara Mjini).

Mbali na Sakaya na Maftaha ambao walikuwa miongoni mwa wabunge wa CUF katika Bunge lililopita, yumo pia mchekeshaji mahiri nchini, Rashid Mwinyishehe, maarufu Kigwendu anayewania Jimbo la Ilala.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Kigwendu aliwania ubunge wa Kisarawe na kuangushwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo.

Katika orodha ya wateule 136 wa CUF, wamo pia waliokuwa wabunge wa chama hicho katika Bunge lililopita, Hamidu Bobali (Mchinga) na Vedasto Ngombale (Kilwa Kaskazini).

Ikiwa wateule hao wote 136 wakipitishwa, CUF itakuwa haina wagombea kwenye majimbo 78 kwa kuwa Tanzania Bara kuna majimbo 214.

CUF kilishika nafasi ya tatu kwa idadi kubwa ya wabunge katika Bunge la 11 lililofungwa Juni 11 mwaka huu, kikitanguliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Wakati CUF ikitoa orodha hiyo, jana Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilikuwa inafanya uteuzi wa wagombea waliokidhi vigezo kuwania urais, ubunge na udiwani katika uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Jumatano Oktoba 28 mwaka huu.

Kwa mujibu wa tume hiyo, kampeni za uchaguzi huo zinaanza rasmi leo na zitafungwa Oktoba 27.

HABARI KITAIFA

## ZSSF yataka waajiri kuwahisha michango

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAAJIRI kisiwani Pemba wametakiwa kutochelewesha michango ya watumishi wao kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), ili kupata mafao ya uzeeni kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari meneja wa mfuko huo, Rashid Mohamed Abdullah, alisema kuna baadhi ya waajiri hasa kwa mashirika binafsi huchelewesha michango hiyo.

Alisema ni wajibu wao kutekeleza kwa kuipeleka michango ya watumishi wao ZSSF, ili watakapostaafu walipwe mafao yao kwa wakati.

Alisema upande wa taasisi za serikali fedha hizo huingizwa kwa wakati, ingawa kwa taasisi binafsi huchelewesha kutokana na kile wanachodai hali ya kibiashara huwa ngumu kwa baadhi ya siku.

"Kwa taasisi za serikali fedha huingizwa kwa moja kwa moja kupitia Wizara ya Fedha, lakini changamoto inakuja pale yanapocheleweshwa ," alisema.

Alisema taasisi ikichelewesha fedha hizo ndani ya siku 15, anatakiwa alipe faini ya asilimia tano ya mchango anaotakiwa kutoa.

## RC Dar aipongeza jumuiya utoaji damu

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge, ameipongeza Jumuiya ya Khoja Shia kupitia programu yake ya "Husayni Blood Drive" kwa kufanikisha uchangiaji damu kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Damu Salama na Hospitali ya Ebrahim Haji.

Uchangiaji damu ulifanyika katika Hospitali ya Ebrahim Haji iliyopo jijini Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha kumbukumbu ya kifo cha mjukuu wa Mtume Muhammed (SAWW), Imam Hussain, lakini ikiwa ni kuendeleza utamaduni wa kujitolea kwa jamii ambao ni msingi mkuu wa ujumbe wa Imam Hussain.

Akizungumza uchangiaji damu, Kunenge aliipongeza jumuiya ya Khoja Shia Ithnasheri kwa tukio hilo lenye upendo kwa kuwa linaenda kuokoa maisha ya watu.

"Nimeambiwa kuwa zoezi hili limefanyika kwa zaidi ya miaka 15 na kukusanya zaidi ya lita 5,000 za damu ambazo zimesaidia kuokoa maisha ya Watanzania wengi, " alisema Mkuu wa Mkoa.

# Kiwanda KACU chaongeza ushindani soko la pamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KUFUFULIWA kwa kiwanda cha uchakataji wa pamba cha Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) kumesababisha kuongeza ushindani wa masomo ya zao hilo kwa wamiliki wa viwanda vya uchakataji wa zao hilo kutoka shilingi 850 kwa kilo hadi 900.

Zainabu Telack, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, aliyabainisha hayo jana wakati wa ziara yake ya siku moja ya kukagua uzalishaji wa kiwanda hicho ambacho kwa siku kinachakata pamba mabero 95, kikiwa na wafanyakazi 140, huku 33 kati ya hao wakiwa wafanyakazi wa kudumu.

Alisema baada ya KACU kufufua kiwanda cha uchakataji pamba kimeongeza ushindani wa soko la pamba kwa wamiliki wa viwanda vya pamba na kununua zao hilo kwa shilingi 900 badala ya shilingi 850 iliyokuwa awali.

**Kila kiongozi wa AMCOS anatakiwa kumsimamia mkulima kutunza pamba na kumkumbusha kanuni 10 za kilimo hicho ili kuendelea kupata pamba safi na ya kutosha.**

Aidha, Telack alisema pasingekuwa na ushindani wa bei hiyo kwenye viwanda vya uchakataji wa zao hilo, wakulima maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Shinyanga wangeendelea kuuza pamba yao kwa bei ya shilingi 850, na kuongeza kuwa chama hicho kimekuwa cha kuigwa nchi nzima.

"Nikupongeze Mwenyekiti wa KACU, Emmanuel Charahani, kwa kununua pamba kilo moja kwa shilingi 900 badala ya 850 iliyopo, umesababisha kuongeza ushindani wa masoko kwa kampuni nyingi na sasa wananunua pamba hii kwa mkulima kiasi cha shilingi 900," alisema Telack.

Telack aliwaka wakulima wa zao hilo kwa kushirikiana na viongozi wa vyama vya msingi (AMCOS) kuhakikisha wanatunza pamba katika hali ya usafi bila kuweka mchanga, maji na mawe ili mwakani bei ya pamba iweze kuongezeka hadi shilingi 1,000 kwa kilo moja.

Kwa upande wake, Charahani alisema, kila kiongozi wa AMCOS anatakiwa kumsimamia mkulima kutunza pamba na kumkumbusha kanuni 10 za kilimo hicho ili kuendelea kupata pamba safi na ya kutosha.

Mhandisi wa kiwanda hicho, Himelius Magege, alisema changamoto wanayoipata katika uzalishaji ni uhaba wa vifungashio, ambavyo vimekwama kufika nchini kutokana na ugonjwa wa Covid-19 na kusababisha kuzalisha marobota 95 kwa siku moja.



Babalishe Saleh Yusuph na msaidizi wake wakiandaa ugali kwa ajili ya kuwauzia wafanyabiashara katika soko la Temeke Vitenari, jijini Dar es Salaam, jana. Sahani moja ya chakula inauzwa kwa 1,000/-. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mlimba wakombolewa huduma za fedha

**Na Mwandishi Wetu,** KILOMBERO

ADHA ya kutekwa na kunyang'anywa fedha zao waliokuwa wakiipata wafanyabiashara katika Halmashauri ya Mlimba Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro, wakati wa kusafirisha umbali wa kilomita 150 ili kuzifikia huduma za kibenki, sasa itabaki kuwa historia baada ya kupata huduma hiyo.

Wakazi hao wameondokana na tatizo hilo baada ya Benki ya NMB kuzindua tawi jipya katika Tarafa ya Mlimba.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Joyce Chaula, akizungumza katika uzinduzi wa tawi hilo jipya, aliupongeza uongozi wa benki hiyo kwa kuwasogezea huduma za kibenki, hatua ambayo pia itawasaidia kuondokana na hali ya kuporwa fedha zao na wakati mwingine kuhatarisha maisha yao.

"Wafanyabiashara wa Mlimba tulikuwa kwenye hatari ya kupoteza maisha pale tunapokuwa tunasafirisha fedha zetu kuhifadhi na kuchukua katika taasisi za fedha umbali wa kilometa 150, lakini sasa baada ya kufunguliwa tawi hili Mlimba sasa tutakuwa salama," alisema Chaula.

Rashid Balali alisema kuwa siku za nyuma katika eneo la Kijiji cha Chita walikuwa wakitekwa kisha kunyang'anywa fedha na kuwasababishia hasara, lakini baada ya kujenga tawi katika eneo la Mlimba wanaamini kuwa watakuwa salama pamoja na fedha zao.

"Tunashukuru sana kwa Benki ya NMB kwa kutujengea tawi katika eneo hili, kwa sababu tutapata fursa nyingi za kifedha ikiwamo kupata mikopo mbalimbali na kuhifadhi fedha zetu tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma," alisema Balali.

Kaimu Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Salie Mlay, alisema ujenzi wa tawi hilo jipya la Mlimba ni utekelezaji wa sera ya serikali ya kuwasogezea huduma wananchi kwa kuwa serikali imekuwa mdau mkubwa wa benki hiyo.

Mlay alisema wataendelea kuimarisha huduma mbalimbali na mpaka sasa wameshafungua jumla ya matawi 226 hapa nchini na kwa mkoa wa Morogoro pekee hilo litakuwa ni tawi la 12, lengo ni kutaka maisha ya Watanzania yaboreke kwa kupata huduma bora za kifedha kutoka katika benki hiyo.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper, alisema katika uzinduzi huo wameweza kutoa mchango kwa jamii wenye thamani ya shilingi milioni tano ikiwa ni mabati kwa ajili ya uwezekaji wa Shule ya Sekondari ya Kalengakelu iliyopo Tarafa ya Mlimba.

Akizindua tawi hilo, Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Ismail Mlawa, alisema ujenzi huo ni sehemu ya ushahidi wa serikali kumletea mwananchi maendeleo ili kuondokana na changamoto zinazomzunguka na kuwataka wafanyabiashara kuitumia benki hiyo kwa ajili ya kufanya maendeleo.

Alishukuru NMB kwa kutoa msaada wa shilingi milioni tano kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Kalengakelu.

# ATCL, NIT kushirikiana kuzalisha wataalamu

**Na Elizabeth Zaya**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Shirika la Ndege nchini (ATCL) wamefufua makubaliano waliyokubaliana mwaka 2012 kati yao ikiwa lengo la kuzalisha wataalamu wengi ambao watasaidia uendeshaji wa ATCL.

Akizungumza baada ya majadiliano kati ya pande mbili, Mkuu wa NIT, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema:

"Kusudi kuu la makubaliano tuliyosaini mwaka 2012 ni kuwezesha taasisi hizi mbili za serikali kushirikiana katika kubuni na kufanya programu mbalimbali za mafunzo, kubadilishana ujuzi unaohusiana na sekta ya anga."

Alisema kupitia Shule ya Anga iliyo chini ya NIT ikitoa mafunzo ya usafiri wa anga, wataweza kuzalisha wataalamu wengi ambao watasaidia uendeshaji wa Shirika la Ndege la Taifa.

**Awali ATCL ilikuwa na ndege mbili, lakini baada ya serikali kuweka uwekezaji mkubwa, ina ndege nane kutokana na serikali kuwekeza zaidi katika shirika hilo.**

Alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 50 ambazo zimewekwa kwa kipindi cha miaka mitano kwa ajili ya kuzalisha wataalamu wa sekta ya anga.

Prof. Mganilwa alisema hayo alipotembelea ATCL akiwa na wajumbe wa bodi wa chuo hicho, ili kuangalia mkataba wa makubaliano waliosaini mwaka 2012 kati ya NIT na ATCL.

Alisema kwa kutumia utaalamu mkubwa wa wataalamu waliopo ATCL, wataweza kuwapa mafunzo Watanzania wengine wanaopenda kujifunza juu ya usafiri wa anga, hivyo wanatarajia kupata wataalamu wengi watakaoendesha shirika hilo liweze kukua.

"Leo hii shirika lina wafanyakazi 575, lakini baada ya miaka miwili ama mitatu litakuwa na wafanyakazi zaidi ya 1,000, ambao watakuwa ni Watanzania, hivyo kulihudumia shirika letu la ndege la Taifa," alisema Prof. Mganilwa.

Alisema awali ATCL ilikuwa na ndege mbili, lakini baada ya serikali kuweka uwekezaji mkubwa, ina ndege nane kutokana na serikali kuwekeza zaidi katika shirika hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa ATCL, Kapteni Said Hamad alilishukuru Baraza la NIT na ATCL kwani walikuwa na majadiliano mazuri, na wamepata faida kubwa sana.

"Moja ya vitu ambavyo tumeamua kuviendeleza ni kuongeza mshikamano kukaa pamoja na kuratibu njia sahihi ambazo zitatuwezesha kuendana na hali halisi ya soko ili kuwezesha NIT kuzalisha vijana ambao wataweza kuja kuwa faida katika shirika la ndege," alisema.



Mkuu wa Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa, akizungumza na waandishi wa habari baada ya wajumbe wa Baraza la Uongozi wa chuo hicho, kutembelea makao makuu ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPB yaijenga shule, madarasa Kibiti

**Na Beatrice Moses**

MATATIZO ya kukosekana kwa ofisi ya walimu na madarasa mawili yaliyokuwa yanaikabili Shule ya Msingi Kikale iliyopo Wilaya ya Kibiti, mkoani Pwani, sasa yamepatiwa ufumbuzi na Benki ya TPB baada ya kugharamia ujenzi wake kisha kuyakabidhi.

Mradi wa ujenzi huo unatajwa kugharimu shilingi milioni 57.8 ikihusisha ujenzi wa madarasa mawili, ofisi ya walimu, madawati 50 na samani za ofisi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi, akizungumza juzi katika hafla ya kukabidhi rasmi mradi huo, alisema benki hiyo ilipokea maombi kutoka katika shuleni hiyo, ikibainisha changamoto zilizopo zikiwamo upungufu wa majengo hasa ya madarasa, ikiwa na wanafunzi takribani 327.

Alisema wanaifahamu shule hiyo ambayo ni kongwe, kwa muda mrefu ilikuwa ikikabiliwa na changamoto hiyo, hivyo kwa kuwa TPB ni miongoni mwa wadau wakubwa wa elimu nchini, na ni jukumu lao ni kusaidia shule hizi zilizopo pembezoni ili kuhakikisha watoto wa maeneo hayo nao pia wanapata elimu katika mazingira bora na salama.

Alibainisha kuwa fedha zilizogharimu mradi huo zimetokana na sehemu ya kiasi cha faida ambayo benki hiyo inapata kila mwaka, hivyo wanaamini madarasa hayo yatatumika vizuri kwa uangalifu ili yaweze kudumu kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Gulamhussein Kifu, alipongeza uongozi wa TPB kwa majengo mazuri na ya kisasa ya madarasa na ofisi katika shule hiyo.

Alibainisha anatambua benki hii inapokea maombi mengi kwa mwaka kwa ajili ya kusaidia jamii katika sekta mbalimbali, ikiwamo elimu na kushukuru Kikale imekuwa miongoni mwa shule zenye bahati kwa mwaka huu kupata msaada huu.

## RITA yasajili watoto mil.5

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), imesajili watoto milioni tano walio chini ya umri wa miaka mitano.

Usajili huo ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa matukio muhimu ya binadamu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Emmy Hudson, alisema mpango wa usajili wa watoto una lengo la kuhakikisha kila mtoto aliye na umri chini ya miaka mitano anasajiliwa na kupata cheti cha kuzaliwa.

Alisema kila mtoto anayezaliwa ni lazima apate nyaraka hiyo ndani ya muda mfupi baada ya uzazi kutokea, utekelezaji wa mpango huo unafanyika kwa kusogeza huduma karibu na makazi ya wananchi bila malipo kutoka ofisi za watendaji kata na vituo vya tiba vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto.

Aliongeza kuwa wamepata mafanikio kwa kusajili zaidi ya watoto milioni tano na kupata vyeti, mpango uliofanyika katika mikoa 18 ambayo inatekelezwa na mpango huo na kupandisha wastani wa watoto walio na vyeti vya kuzaliwa kutoka asilimia 13 na sasa kufikia asilimia 49.


Alisema kati ya watoto waliosajiliwa, asilimia 50.1 ni wanaume na 49 ni wanawake.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Mbeya, Songwe, Mwanza, Iringa, Njombe, Geita, Shinyanga, Mtwara na Lindi.

## Ukimwona mtoto huyu toa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

MTOTO Magreth Mgutu (15), anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao Mbezi Kwa Yusufu jijini Dar es Salaama na kwenda kusikojulikana.



Mama yake mkubwa, Jenifa Onyango, alisema, alitoweka Agosti 16, mwaka huu, na kwamba taarifa za kupotea kwake zipo Kituo cha Polisi Kimara.

"Nimefungua jalada namba KMR/RB/9276/2020, na ninawaomba wasamaria wema watakaomwona watoe taarifa kituo cha polisi na pia watujulishe kwa namba 0784- 247799 na 0763-981819," alisema Jenifa.

Amesema, siku ya tukio mtoto huyo alikuwa ametumwa gengeni jioni, lakini akachelewa kurudi hadi saa tatu usiku, hali iliyosababisha yeye (Jenifa) kuanza kumfuatilia wakawa wamepishana njiani.

"Baada ya kupishana, alifika na kuacha kwa jirani vitu nilivyomtuma na kumuaga kwamba anatoka kunifuatilia, na tangu wakati huo hajaonekana licha ya kumtafuta maeneo mbalimbali," alisema.

## Uwazi kura, kujisogeza karibu kulivyochagiza vijana kutia nia



Ukurasa 12




Ukurasa 13

## NI UCHAGUZI WA WANAWAKE 2020

siasa
JUMATANO JAGOSTI 26, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe


# Muungano wa vyama,mgombea mmoja unavyokausha ruzuku



Tundu Lissu



Benard Membe



John Shibuda

**Na Ani Jozeni**

UWEZEKANO wa kuunganisha vyama kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao ni agenda ambayo imeshindikana.

Mipango ya kuunganisha au kushirikiana kwenye uchaguzi haujapewa kipaumbele wakati wa maandalizi ila hujitokeza mwishoni wakati wa kuchukua fomu kupata wadhamini zinazotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Viongozi wa CHADEMA, ACT-Wazalendo hawajalipa nafasi suala hilo mwaka huu.

Kwa upande mmoja juhudi hizo zilikuwa zinaendana na jitihada za kuunganisha nguvu ili kuwa na uwezo zaidi kupambana na CCM. Aidha, kwa upande mwingine jitihada hizo ziliendeleza mambo ya uchaguzi mkuu uliopita.

Kwa upande huu wa pili, zilisikika sauti kutahadharisha kuwa asije kuwekwa mgombea wa pamoja ambaye baadaye ataukimbia upinzani na kurudi 'nyumbani,' CCM hoja ambayo ilikuwa inamlenga mtia nia muhimu upinzani.

Yeye mwenyewe alielewa suala hilo na katika mkutano wa kumpatia kadi, akakiambia ACT-Wazalendo kuwa alifukuzwa.

Ina maana kuwa anazo 'kinga' za kutorudi CCM ukilinganisha na mgombea wa CHADEMA 2015 ambaye pia aliwakilisha Chama cha Wananchi (CUF), na ndiyo hapo uhusiano na uchaguzi mkuu uliopita unapoanzia. Kwanza hapakuwa na suala lolote mwaka huu wa kuijumuisha CUF katika kutafuta mgombea wa pamoja kwani ilikatika vipande viwili, kipande kikubwa cha Zanzibar kikabakiza utii kwa Seif Shariff Hamad, ambaye ACT-Wazalendo imempa uenyekiti wa taifa wa chama, huku mwanzilishi Zitto Kabwe akiwa kiongozi mkuu.

Kundi jingine likiendelea kuwa chini ya Mwenyekiti wa Taifa, Profesa Ibrahimu Lipumba, ambaye alirudishiwa uongozi huo baada ya kuupigania mahakamani na kwa ofisi ya msajili wa vyama.

Mapema alipojiunga ACT-Wazalendo alipewa nafasi ya mshauri mkuu wa chama, ambayo pia alipewa aliyekuwa mgombea urais 2015 CHADEMA, Edward Lowassa.

Siyo rahisi kuona jinsi ambavyo juhudi za kuunganisha nguvu za vyama hivyo vya upinzani zingeweza kufanyika mapema, kwani hakuna uchaguzi mkuu ambako suala hilo limeweza kujadiliwa mapema na kukubaliwa. Mara zote suala hilo linategemea nguvu za vyama husika wakati uchaguzi mkuu unakaribia, yaani matayarisho yake yote hasa kuhusu mgombea urais mtarajiwa, halafu ndiyo iangaliwe kama anafaa kuwa mgombea wa pamoja wa upinzani. Sababu ni kupata viti vingi vya bunge na si ajabu hata kushinda.

Ukiangalia kilichotokea katika wiki mbili au tatu za mwisho za kutafuta wagombea urais wa kila chama, kulikuwa na jitihada za kupatikana kada wa siku nyingi CCM na waziri mwandamizi kwa miaka tisa, Bernard Membe, kujiunga ACT-Wazalendo. Kielelezo cha hatua hizo ni kuwa kuelekea mwisho wa mwaka jana Zitto Kabwe, alieleza nia yake ya kugombea urais mwaka huu, ambayo aliiweka pembeni wakati matayarisho ya kutafuta mgombea wa urais wa chama hicho yakianza.

Hapakuwa na juhudi zozote wakati huo za kushirikiana na CHADEMA kwa suala hilo, kwani mtafutwa huyo hakuonekana kuwa na nguvu miongoni mwa wapiga kura au mvuto kwa wana-CCM kwa kufananishwa na Lowassa wakati ule.

Ndiyo maana bado kuna maswali kwanini juhudi hizo zikaanza kusikika baada ya kada huyo wa siku nyingi kuhamia ACT-Wazalendo, kama ni kujihusisha na juhudi za kuleta umoja upinzani kama sehemu ya 'uwazi na ukweli,' kuwaridhisha wanachama au wafuasi wa CHADEMA, au ulikuwa ni mkakati halisi wa kuweka nguvu pamoja.

Hapo kuna kitendawili lakini kwa jumla mazingira hayakuwa muafaka kwa juhudi hizo ndani ya CHADEMA kwani wafuasi wake walikuwa wana shauku kubwa ya ujio wa makamu mwenyekiti Bara, Tundu Lissu kutoka ng'ambo.

Halafu bado ushawishi wa baadhi ya makada waandamizi kugombea ulikuwepo, hivyo ajenda ya kuunganisha nguvu na ACT-Wazalendo haikuinuka.

Kwa upande fulani ilionekana kuwa kuunganisha nguvu na ACT-Wazalendo ingekuwa ni aina ya suluhu katika CHADEMA kwani mvutano wa kuchukua fomu kutaka kugombea ulikuwa si lelemama.

Tatizo ambalo halijazungumziwa ni ile hali ya 'kugeuziwa kibao' uchaguzi mkuu 2020 ukilinganisha na kilichotokea baada ya uchaguzi mkuu 2015.

Licha ya kuwa kuna tatizo la uelewano na kufikia mkataba endelevu wa ushirikiano kwa mapana kiwango fulani kutokana na kuwa na mgombea mmoja, mazingira ya kisheria pia siyo rafiki wa mkakati kama huo. Inabidi kujituma kwa njia isiyo ya kawaida kushirikiana.

Tatizo la msingi ni kuwa kanuni za uchaguzi mkuu zinamtambua mgombea kuwa ni wa chama fulani, na kama kuna vyama vilivyomuunga mkono inakuwa ni shauri lao wenyewe, na siyo suala la kisheria (kuhusiana na nafasi ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa) .

Ofisi hiyo ambayo inahusika kugawa ruzuku kwa vyama vya siasa inagawa ruzuku hiyo hasa kwa msingi wa kura za urais, sababu mojawapo ni kuwa majimbo ya uchaguzi yanalingana na idadi ya watu, hivyo kulinganisha wingi wa viti bungeni kuna walakini. Ina maana chama ambacho hakina kura za urais kinaweza kupata shida ya ruzuku hapo baadaye.

Ndicho kilichotokea baada ya uchaguzi mkuu 2015 ambako mgombea wa urais alikuwa wa pamoja kati ya CHADEMA na CUF, halafu katika kugawa ruzuku, CUF ikawa inapata fedha kiduchu zaidi kipindi cha miaka mitano iliyofuata kutokana na kutokuwa na mgombea urais.

Wakati wa mgogoro kuhusu kurudi kitini mwenyekiti wa taifa Profesa Ibrahim Lipumba, hoja ya makada Bara, na hasa vijana ilikuwa ni kutokuwapo faida ya kuweka mgombea kwa pamoja.

Takwimu mojawapo iliyokuwa inatolewa ilidai kuwa wakiwa na wabunge wawili uchaguzi mkuu 2010 huku Profesa Lipumba akiwa wa tatu matokeo ya kura za urais akiwa na kura zaidi ya milioni 1.8,chama kilikuwa kinapata ruzuku ya Sh. milioni 600 kwa mwaka.

Lakini, uchaguzi mkuu 2015 ikiwa na wabunge takriban 10 (kutoka Bara) wakati mgombea urais akiwa wa pamoja na CHADEMA, ruzuku inapungua hadi Sh. milioni 200 na kuona kuwa ugombea wa pamoja ni hasara.

# Uwazi kura, kujisogeza karibu kulivyochagiza vijana kutia nia



Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM wakihesabu kura za mgombea urais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi , jijini Dodoma , **PICHA MTANDAO.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MWAKA 2015 kwa vijana kutia nia ya kugombea ubunge ilikuwa sababu tosha ya kupata ajira au kuteuliwa na Ikulu katika nyadhifa mbalimbali za uongozi wa umma.

Pengine hilo ndilo limekuwa chanzo cha kuwachagiza vijana lukuki kutia nia ya ubunge kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi mwaka huu.

Tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi nchini, mchakato wa uchaguzi wa mwaka huu umetoa tafsiri ya kukomaa kwa demokrasia, ndani ya chama tawala, kufuatia wanachama wake hususani vijana wasomi kutia nia ya kuwania ubunge katika majimbo mbalimbali.

Wasomi hao wamesukumwa kuomba ridhaa ya kupeperusha bendera ya CCM katika kinyang'anyiro cha ubunge, viti maalumu na udiwani, kitakachohitimishwa na uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka huu.

Wagombea hao wanatazama matokeo ya mwaka 2015 yaliyowapaisha miongoni mwa walioshiriki kwa dhati kuwania nafasi za uwakilishi kwa wananchi na kura zao kutotosha kuangukia katika uteuzi mbalimbali.

Baada ya uchaguzi huo, Rais John Magufuli, aliwateua baadhi yao katika nafasi mbalimbali watiania hao wa nafasi ya ubunge na miongoni mwao ni Swertberth Nkuba, aliyejitokeza mwaka huo jimbo la Kahama Mjini, awali aliteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Tabora.

Yuko pia Godwin Kitonka, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe na Pius Luhende mwenye wadhifa kama huo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, hata hivyo utezi wa Luhende, ulitenguliwa baada ya kutuhumiwa kwenye kesi ya mauaji. Aidha yupo na Zabroni Bugingo aliyetia nia jimbo la Sengerema, aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Kilwa. Matokeo hayo yalibainisha kuwa huenda kuonyesha nia ni njia rahisi ya kupata madaraka pengine makubwa serikalini.

**HAMASA NA CHACHU**

Hapana shaka matokeo hayo, yamekuwa chachu kwa wasomi wengi katika mwaka huu wa uchaguzi wa 2020, kutia nia katika nafasi za ubunge, huku wakiwa na matarajio ya kupata fursa kama za uchaguzi uliopita wa mwaka 2015.

Vijana hao huenda wanaichukulia siasa kama njia ya kuwafikisha katika ndoto zao za kufikia mafanikio yao kimaisha. Siasa wametambua ni ajira hasa ukiwa ndani ya chama tofauti na ilivyokuwa hapo mwanzo.

Ukitazama utitiri wa watiania kupitia CCM, ambao wamekisaidia chama kupata mapato kutokana na ada ya uchukuaji fomu kwa wasomi hao, huenda ulilenga katika kupata fursa za ajira ama uteuzi wa nafasi mbalimbali kwa kudra za Ikulu.

Pamoja na kudaiwa chama kurejeshwa kwa wanachama na kuthibitishwa na matokeo mazuri ya utekelezaji wa ilani unofanywa na awamu ya tano, kuvutia vijana kutokana na kuwapa fursa kubwa ya uongozi, lakini yaliyojiri baada ya uchaguzi wa mwaka 2015.

Wakati wa mchakato wa kumtafuta mgombea wa nafasi ya urais kupitia Zanzibar,Rais Magufuli alisisitiza kuwa kuhesabu kura za maoni ndani ya chama kuwe wazi kwa kila mgombea na wajumbe na hiyo ikawa moja sababu ya vijana kujitokeza kwa wingi kwa mwaka huu.

> Mwaka 2017 nilijitokeza kugombania nafasi ya ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa CCM wilaya na kushinda kwa kupata kura 856 na kuwashinda wasiokuwa walemavu. Hivyo tukijitokeza kugombea tunaweza tukashinda "Anasema Mkanjiwa.

Wilaya ya Kahama mkoa wa Shinyanga ni moja ya maeneo waliyojitokeza vijana wengi kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya CCM ukilinganisha na watu wazima walijitokeza uchaguzi mkuu uliopita wa mwaka 2015.

**SAUTI YA KATIBU CCM**

Emmanuel Mbamange, ni Katibu wa CCM Wilaya ya Kahama na msimamizi wa uchaguzi ngazi za chama, anasema mwaka huu wa 2020 vijana wengi wamejitokeza kuomba ridhaa katika majimbo ya Kahama Mjini, Ushetu na Msalala ukilinganisha na uchaguzi wa mwaka 2010 na 2015.

Anasema kupiga kura za wazi, kuzihesabu kura mbele ya wagombea na wajumbe na kila mgombea kupewa kura yake mkononi na kumewavutia vijana kujitokeza kwa wingi na kujiona wanaweza kuthubutu na kuchaguliwa.

Pia Mbamange anasema kuwa, kipindi cha nyuma nafasi za ubunge na madiwani zilitafsiriwa kama eneo la watu wazima wenye fedha na kwa mtu asiyekuwa na pochi nene ilikuwa hawezi kuthubutu kuomba ridha, lakini kwa mwaka huu imekuwa tofauti na kuwavutia vijana wengi.

Anaongeza: "Vijana wengi waliojitokeza kuomba ridhaa kwenye nafasi ya ubunge na kupata kura sifuri, hawatambuliki na wajumbe kwenye mashina au kata zao wanazotokea. Niwaombe wajenge tabia ya kushiriki shughuli za kijamii kwenye maeneo yao kwa kutengeneza majina midomoni mwa wananchi."

Mbamange anaongeza kuwa vijana waliojitokeza kuchukua fomu za kuomba ridhaa walikuwa 103 katika majimbo ya Kahama Mjini, Ushetu na Msalala, huku Kahama mjini wakiwa 61, Msalala 42 na wanawake vijana katika majimbo hayo wakiwa 11.

**KUDHIBITI RUSHWA**

Aidha Mbamange anasema kuwa, serikali kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama na Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa ( walidhibiti kwa kiasi kikubwa utoaji wa rushwa kwa wagombea maeneo mengi na kufanya uchaguzi kuwa na sura mpya ukilinganisha na uchaguzi uliopita.)

Anasema malalamiko ya baadhi ya wagombea wa nafasi ya ubunge na udiwani juu ya rushwa yaliyokuwa ya yakiripotiwa ndani ya chama mengi yalikuwa ya kufikirika na walipofuatilia kwa ukaribu na kujua kinachoendelea yalikuwa sio ya ukweli.

**MBAMANGE ANAENDELEA KUSEMA:**

"Hatuwezi kusema uchaguzi wa kura za maoni ndani ya chama haukuwa na rushwa ila ilipothibitika mgombea wa nafasi ya ubunge na udiwani ametoa rushwa maofisa wa TAKUKURU walimkamatwa kwa mahojiano na uchunguzi zaidi."

**HAMASA WENYE ULEMAVU**

Mwenyekiti wa Shirikisho wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu wilayani Kahama mkoani Shinyanga (SHIVYAWATA), Michael Mkanjiwa, anasema wakati wa kuchukua fomu za kuomba uteuzi aliwataka watu wenye ulemavu hasa wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu.

Anasema Wilaya ya Kahama ina zaidi ya watu wenye ulemavu 3,000 lakini wanaojitokeza kugombania nafasi za uongozi mbalimbali za udiwani na ubunge Msalala, Ushetu na Kahama Mjini ni idadi ndogo ukilinganisha na waliopo.

"Mwaka 2017 nilijitokeza kugombania nafasi ya ujumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa CCM wilaya na kushinda kwa kupata kura 856 na kuwashinda wasiokuwa wa walemavu. Hivyo tukijitokeza kugombea tunaweza tukashinda "Anasema Mkanjiwa.

Anaongeza: "Tunataka uchaguzi huu tupate viongozi wa aina mbalimbali wakiwamo wenye ulemavu ambao watatusemea matatizo yetu hasa viongozi wanawake kwana wanaweza kufanya mambo makubwa kwenye nchi hii ukilinganisha na wengine."

Aidha, Mkanjiwa anasema, wengi wao wanashindwa kujitokeza kwenye uchaguzi kugombania nafasi mbalimbali kwa kuogopa kuchekwa na kutoungwa mkono na wananchi kwa madai viongozi wenye ulemavu hawawezi kuwa watendaji bora.

Kwa kipindi cha nyuma wenye ulemavu walishindwa kujitokeza na kugombea nafasi za uongozi kutokana na kukithiri kwa vitendo vya rushwa ndani ya vyama vya kisiasa, lakini kwa mwaka huu hali imekuwa tofauti na kila mmoja ana haki ya kuwa kiongozi kupitia nafasi ya kuchaguliwa, anaongeza mwenyekiti huyo.

# NI UCHAGUZI WA WANAWAKE 2020

## •Zaidi ya 100 wametinga majimboni
## •Vyama viwili vyawateua ugombea urais




Queen Sendiga



Cecilia Mwanga

**Na Sabato Kasika**

TOFAUTI na miaka ya nyuma, safari hii vyama vya siasa ni kama vilikuwa vinashindana katika mchakato wa kupata wagombea ubunge wanawake kwenye majimbo mbalimbali Tanzania Bara.

Hii inatokana na ukweli kwamba, vyama vyote vikubwa vimeteua wanawake wengi watakaowania nafasi hiyo kwenye kampeni ambazo zinatarajia kuanza rasmi leo, ili kuwakilisha wananchi katika chombo cha kutunga sheria.

Kwa mujibu wa idadi iliyotolewa na baadhi ya vyama hivyo CHADEMA, kina wagombea wanawake 40 na kufuatiwa na CUF kilichoteua wanawake 34.

Mbali na hivyo, CCM na ACT-Wazalendo, vimefungana kwa kila kimoja kuteua wanawake 16 kuwania ubunge katika majimbo mbalimbali ya uchaguzi.

Hivyo ni wazi kwamba, kwa mara ya kwanza mwaka huu, Watanzania watawashuhudia wanawake wengi wakiomba kura ili wachaguliwe kuwa wabunge wa majimbo badala ya kutegemea viti maalum tu.

Wakati vyama hivyo vinne vikichuana kuteua wanawake wengi kugombea majimboni, vyama vya Demokrasia Makini na cha Alliance for Democratic Change (ADC), vimeteua wanawake kuwania urais. Kinamama hao ni Queen Sendega ,anagombea urais kupitia ADC wakati Cecilia Mwanga, anaipeperusha bendera ya Demokrasia Makini.

Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), kimemteua Queen Sendinga katika nafasi hiyo, na kuweka wagombea wanawake katika majimbo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam, huku Cecilia Mwanga akiwakilisha Chama cha Demokrasia Makini kwenye nafasi ya urais.

**UCHAGUZI WA AWALI**

Kumbukumbu zinaonyesha kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005, CCM kulikuwa na wagombea ubunge wanaume 213 wakati kinamama walikuwa ni 19 ambao ni sawa na asilimia 18. Chadema wagombea wanaume 133 waliowania ubunge huku wanawake wakiwa 11, sawa na asilimia nane, aidha, CUF walisimamisha wagombea wanaume 200 huku wanawake wakiwa 13, sawa na asilimia sita, na NCCR Mageuzi wanaume 63, wanawake nane, sawa na asilimia 11.

Uchaguzi mkuu uliofuata wa mwaka 2010, CCM iliweka wagombea ubunge wanaume 215 na wanawake 24 katika majimbo

> Kwa mfano katika uchaguzi huo CCM, uteuzi wake kwa wanawake ulikuwa ni asilimia tisa, wakati CHADEMA ulikuwa ni asilimia sita, CUF ikiwa ni asilimia 11 na ACT-Wazalendo asilimia 15," anasema Liundi.

wakiwa ni sawa na asilimia 10 wakati Chadema iliweka wanaume 154 na wanawake 25 sawa na asilimia 14.

Kwa upande wa CUF, iliweka wagombea ubunge wanaume 168 na wanawake 14 ambao ni sawa na asilimia nane, huku NCCR Mageuzi ikiwa na wagombea 52 na wanawake 15 ambao ni sawa na asilimia 22.

**UWIANO**

Kumekuwapo na jitihada zinazofanywa na wadau wa kutetea haki za wanawake nchini, kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake, ili wajitokeze kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu.

Miongoni mwa jitahada hizo ni mafunzo kuhusu mada za masuala ya kisiasa yanayozunguka uchaguzi, jukumu la bunge na mabaraza ya mitaa, na umuhimu wa sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.

Katika kufanikisha hilo, wadau hao walishaandaa Ilani ya Uchaguzi ya Wanawake na kuisambaza kwa vyama vya siasa itumike katika mchakato wa kupata wagombea kwa uwiano sawa kati ya wanaume na wanawake.

Baadhi ya wadau hao ni wale walioshirikiana na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na wanawake na makundi mbalimbali, yanayotetea haki zao na watoto wa kike kuandaa ilani hiyo.

Ilani hiyo inahamasisha wanawake, ambao pia ni wapigakura wakatae kuendelea kutumiwa kama wapigadebe, wasindikizaji katika kampeni, waburudishaji bali wachaguliwe kuongoza.

Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi, anatolea mfano uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, kwamba vyama viliteua wagombea wanawake wachache, hali inayohitaji kufanyiwa mabadiliko.

"Kwa mfano katika uchaguzi huo CCM, uteuzi wake kwa wanawake ulikuwa ni asilimia tisa, wakati CHADEMA ulikuwa ni asilimia sita, CUF ikiwa ni asilimia 11 na ACT-Wazalendo asilimia 15," anasema Liundi.

**MWELEKEO MPYA**

Mdau mwingine wa kutetea haki za wanawake, Justa Mwaituka, Mkurugenzi Mtendaji wa asasi ya KIWOHEDE, anasema, uteuzi wa wanawake wengi katika majimbo ni mwelekeo mzuri.

"Angalau sasa tunaanza kuona mwanga, kuna mwelekeo mzuri, tofauti na kule tulikotoka ambapo wanawake walikuwa waoga, hawajiamini, lakini bado tunataka 50 kwa 50," anasema Mwaituka.

Anasema, kilichobaki sasa ni wanawake wenyewe kuungana kwenye kampeni kuhakikisha wanawachagua wale walioteuliwa na vyama kuwania ubunge wa majimbo na pia kuwaunga mkono kwa hali na mali.

Mwaituka anasema, kampeni zina gharama kubwa, hivyo wanawake hawana budi kuungana na kuwasaidia wenzao wanaowania urais, ubunge na udiwani, bila kujali vyama wanavyowakilisha ili hatimaye waibuke na ushindi.

**WAPIGAKURA**

Tume ya Uchaguzi (NEC), imeshatangaza kwamba, idadi ya wapigakura waliojiandikisha kupigakura 2020 ni milioni 29.1 idadi ambayo inaonyesha ongezeko kuliko uchaguzi uliopita.

Wote waliojiandikisha wakijitokeza kupiga kura mwaka huu, au wachache wakashindwa kushiriki, itakuwa ni rekodi bora tofauti miaka ya nyuma ambayo wengi hawakushiriki.

Kwa mfano, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, wapigakura waliojiandikisha walikuwa milioni 10.08, lakini waliojitokeza kuchagua viongozi walikuwa ni milioni 8.51 ambao ni sawa na asilimia 84.4.

Kwa mjibu wa taarifa za NEC uchaguzi wa mwaka 2005, waliojiandikisha kupiga kura walikuwa milioni 16.4 waliojitokeza siku ya uchaguzi walikuwa milioni 11.36 sawa na asilimia 69.3 na uchaguzi mkuu wa

2010, idadi ya wapigakura waliojiandikisha ilikuwa ni watu milioni 20.1 wakati waliojitokeza katika uchaguzi walikuwa milioni 8.6 wakiwa ni sawa na asilimia 42.84 ya wapigakura waliojiandikisha.

Halikadhalika zinaonyesha kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, kati ya watu zaidi ya milioni 23 walioandikishwa kupiga kura, waliojitokeza walikuwa ni milioni 15.6 ambao ni sawa na asilimia 67. Hivyo mwaka huu huenda kukawa na mwamko zaidi.

# LÉOPOLD SÉDAR SENGHOR:

- Mfungwa aliyeibuka kuwa rais
- Aliasisi vuguvugu la Waafrika kujithamini



**Na Mwandishi Wetu**

LÉOPOLD Sédar Senghor husomwa 'Leopod Seda Seng'oo' anachukuliwa kama mmoja wa viongozi na wasomi wakuu wa Afrika. Tena ni mwandishi na mshairi maarufu.

Baada ya kufungwa jela wakati wa vita vya pili vya dunia kutokana na kazi ya ushairi iliyokosoa na kuweka wazi mateso ya Waafrika kwenye kambi za askari, alikuja kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Senegal.

Senghor alikuwa Mwafrika wa kwanza aliyechaguliwa kuwa mwanachama wa Académie française. Kabla ya uhuru wa nchi yake aliunda chama cha Umoja wa Kidemokrasia wa Senegal démocratique sénégalais. Wengi wanamhesabu kati ya wataalamu muhimu zaidi wa Afrika katika karne ya 20.

Senghor alizaliwa katika kijiji cha Joal kilichowahi kuwa kati ya vituo vya kwanza vya wafanyabiashara kutoka Ulaya na pia kitovu cha misheni za Kanisa Katoliki kwenye pwani ya Senegal. Baba yake alikuwa mfanyabiashara mzalendo, mama yake mke wa tatu wa baba yake ambaye imani yake ilimruhusu kuoa wake wengi.

Alipokuwa na umri wa miaka nane alianza kusoma shule ya Kikatoliki na kuendelea na masomo kwenye seminari ya Mapadri wa Shirika la Roho Mtakatifu na baadaye aliacha na kujiunga na shule za kawaida. Baadaye alikwenda Ufaransa kwa masomo ya chuo kikuu.Kwenye Chuo Kikuu cha Paris alihitimu lugha na kupewa nafasi ya kufundisha kwenye vyuo vya Tours na Paris. Mwaka 1932 alipata uraia wa Ufaransa.

Tangu siku zake masomoni alikuwa na urafiki na mwanazuoni Aime Cesaire mwenye asili ya Afrika na Caribbean ambao kwa pamoja waliasisi vuguvgu la "the negritude" ambalo ni uamsho wa Waafrika kujitambua na kufurahia uwepo wao na kuendeleza utamaduni wa "Watu Weusi" kama utamaduni wa pekee na muhimu, tofauti na utamaduni wa Kizungu ambao waliona kama unawadhalilisha.

Mwaka 1945, baada ya vita vikuu vya pili na ushindi wa Ufaransa, Senghor alijiunga na chama cha Kisoshalisti akachaguliwa kuwa mbunge, kunako mwaka 1960 alichaguliwa kuwa rais wa kwanza wa Senegal akaendelea kushika nafasi hiyo hadi mwaka 1980 alipong'atuka kwa hiari.

**URAIS**

Alikuja kuwa Rais wa Jamhuri ya Senegal mnamo Septemba 1960, baada ya kufanya kazi kama mwandishi wa habari, miongoni mwa mambo mengine mengi aliyojishughulisha nayo. Alikuwa iongozi wa taifa hilo la Senegal lilitawaliwa na Wafaransa kwa miongo miwili yaani kuanzia 1960 hadi 1980. Alifariki Desemba 20, 2001, akiwa na miaka 95, nchini Ufaransa.

**MAMBO MUHIMU**

Senghor alikuwa mpenda amani, ubinadamu na katika kazi yake alikuwa ni mwenye kuamini juu ya kutenda jambo kwa ukamilifu wake. Ni mwanazuoni msomi mwenye kupenda sana kujifunza lugha tofauti. Mnamo mwaka 1984, alikuwa ni mwandishi wa kwanza mweusi kuchaguliwa kama mwanachama wa Académie française -Baraza Maarufu la Lugha Ufaransa.

Bila ya pingamizi, alikuwa ni kiongozi wa kwanza barani Afrika kujiuzulu kwa hiari yake mwenyewe bila shinikizo la umma.

UJAMAA WA KIAFRIKA

Rais huyu wa zamani wa Senegal ni kiongozi aliyeshiriki kuasisi na kuamsha vuguvugu la Waafrika kujiamini , kujikubali, kufurahia Uafrika wao na kuondokana na fikra za kikoloni na kibaguzi zilizolenga kuwafanya wajione kuwa ni duni na kubaguliwa kuwa ni weusi.

Alikuwa amewalenga Waafrika wa makoloni ya Kifaransa -Francophone, ambao walikuwa wanabaguliwa na kuonekana kama jamii ya kiwango cha chini, akiliita vuguvugu hilo maarufu kama negritude.

Anahusika na ujenzi wa ujamaa wa Kiafrika (African Socialism) ambayo imeanzia kwenye vuguvugu hilo la negritude.

Senghor hawezi kutenganishwa na Wanamajumuni wa Afrika waliotetea na kusisitiza muungano, umoja na udugu wa Afrika akiwamo Kwame Nkrumah wa Ghana, Mwalimu Julius Nyerere, Nelson Mwandela wa Afrika Kusini, Milton Obote wa Uganda, Nnamdi Azikiwe wa Nigeria , Sékou Touré wa Guinea na William Tubman of Liberia.

Wote waliamini kuwa ukombozi kamili wa bara la Afrika ni umoja na watu wake wawe wamoja hivyo wanahitaji taasisi moja imara kuongoza Afrika dhidi ya wadhalimu na wahujumu wa bara hili nao ni Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU).

Senghor alikuwa anaamini katika falsafa ya kuchagua na kukubaliana masuala ya utendaji na falsafa za kisiasa kutoka mirengo mbalimbali badala ya kukumbatia jambo au dhana moja kiongozi au kundi fulani linaloamini kwenye mambo na taratibu zinazohusu ujenzi wa taifa.

Anatajwa kuwa ni kiongozi aliyekuwa anaamini katika chama kinachoongoza kufanya uamuzi muhimu ya maendeleo ya taifa na kuwa msemaji wa wananchi kwenye masuala muhimu.

Kadhalika Senghor alikuwa anaamini katika kuhakikisha usawa kwenye uzalishaji, umiliki na mgawanyo wa keki ya taifa kwa misingi ya usawa.

Rais wa Senegala kuanzia 1960 hadi 1980 aliamini katika ujamaa wa Afrika unaowekeza kwenye kuyaheshimu na kuyakubali mawazo, utamaduni na tunu za Mwafrika.

**KUKOSOLEWA SENGHOR**

Kati ya mwaka 1962 na 1968, Léopold Sédar Senghor anadaiwa kufanya makosa kadhaa ya kisiasa wakati akijaribu kulinyamazisha vuguvugu la Popular Front la nchini Senegal.

Mwaka 1968 alikabiliana na kundi la wasomi la vuguvugu lililokuwa likifuata muongozo wa Marxism, mwanafalsafa wa Kijerumani wa karne ya 19 ambaye kazi zake zilihusisha nadharia za kiuchumi, na siasa za kijamaa na kikomunisti zikilenga ukandamizaji wa kibeberu.

***MITANDAO***



# Umwonapo mtoto huyu toa taarifa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWANAFUNZI wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Makole jijini Dodoma, Catherin Ngalya (15), amepotea katika mazingira ya kutatanisha kwa takribani siku 20, baada ya kuondoka nyumbani bila kuaga mtu yeyote.

Akizungumza katika ofisi za gazeti hili jana jijini Dodoma, baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Aloyce Matibu, alisema kuwa wamejaribu kumtafuta kila eneo bila mafanikio.

Matibu, alisema kuwa mtoto wake alitoweka nyumba Agosti 8, mwaka huu na kuelekea kusikojulikana hali ambayo imewalazimu kuacha shughuli nyingine na kuanza kumtafuta.

Alisema kabla ya kutoroka nyumbani Catherin, alikutwa na simu ya mkononi na mama yake ambaye alimpokonya na kumhoji baadhi ya maswali.



"Siku moja kabla ya kuondoka nyumbani mwanangu alikamatwa na simu ya mkononi na mama yake akamuhoji kuwa ameipata wapi halafu yeye akaenda kazini asubuhi, aliporudi mchana hakumkuta nyumbani hadi leo hii hajarudi," alieleza Matibu.

Pia alisema mtoto huyo aliondoka na begi la nguo zake na katika kumfuatilia walipata taarifa kuwa yupo katika Kijiji cha Mbande wilayani Kongwa mkoani hapa.

"Baada ya kupata hizo taarifa kuwa yupo Mbande Kongwa, tulifunga safari na kuweka kambi kwa zaidi ya wiki moja bila kumpata," alisema Matibu.

Aidha, Matibu alisema kuwa baada ya kuzunguka kila eneo bila mafanikio, walitoa taarifa katika kituo cha polisi Kisasa jijini Dodoma na kupatiwa RB namba DOM/ ILIS/RB/566/2020.

Aliwaomba watakaomwona mwanafunzi huyo, watoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo jirani au wapige simu katika namba yake, 0769366888.

"Tunawaomba sana watu watakaomwona watupe taaarifa kwa namba hiyo hapo, lakini watoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kwani binti yetu bado mdogo sana na anahitaji kuendelea na masomo ili atimize ndoto zake," alibainisha Matibu.

# Watumishi watano kortini madai uhujumu uchumi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imewafikisha mahakamani watumishi watano wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Watumishi hao wanashtakiwa kwa matumizi mabaya ya fedha na kuisababishia Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa hasara ya Sh. milioni 149.8.

Makosa hayo ni kinyume cha Kifungu cha Sheria Namba 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema watuhumiwa hao walikuwa ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

Aliwataja watuhumiwa ni Fanuel Senge (67), aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji, Ignace Chacha (48), aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, Joel Nsekela, aliyekuwa Ofisa Mipango.

**TAKUKURU inawakumbusha watumishi wa umma kwamba jinai haifi, unaweza kutenda kosa leo likaja kujulikana hapo baadaye, inawezekana ukawa hukumbuki, lakini uchunguzi ukifanyika unafikishwa mahakamani bila kujua.**

Wengine ni Moses Wambura (38), Gerald Masawe aliyekuwa Meneja mradi wa ujenzi wa ukumbi wa kibiashara wa Wilaya ya Mpwapwa.

Kibwego alisema kuwa uchunguzi wa TAKUKURU unaonyesha watu hao Septemba 12 na Desemba 2013, walitoa zabuni ya ujenzi wa ukumbi wa biashara yenye thamani ya Sh. milioni 356 kwa kampuni ya Magoma and Ryakitimbo Contractor LTD bila kufuata taratibu za manunuzi ya umma kwa bodi ya zabuni. Pia alisema uchunguzi umeonyesha mkandarasi alilipwa jumla ya Sh. milioni 149.8.

Vilevile, TAKUKURU wamewapandisha mahakamni aliyekuwa Ofisa Elimu Msingi, Abubakary Adam (57) na aliyekuwa Ofisa Elimu Ufundi wote wa Halmashauri ya Chamwino kwa kosa la kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri kinyume cha sheria.

Watuhumiwa hao wamefunguliwa mashtaka 8 ya kughushi na shtaka moja la ubadhirifu kinyume cha kifungu cha sheria namba 28.

Kibwego alisema uchunguzi wa TAKUKURU unaonyesha Agosti na Oktoba 2015, watuhumiwa walighushi nyaraka mbalimbali kinyume cha taratibu na kujipatia Sh. milioni 3.5 ambazo walidai walizitumia kutengeneza kasiki katika shule 12, zilizopo katika halmashauri hiyo.

Kibwengo alisema kesi hiyo itatajwa tena Septemba 24, 2020 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mpwapwa chini ya Hakimu Nuru Nasari.

Aliwaonya watumishi wa umma kuwa wanapaswa kuwa makini katika utendaji wao wa kazi za kila siku.

"TAKUKURU inawakumbusha watumishi wa umma kwamba jinai haifi, unaweza kutenda kosa leo likaja kujulikana hapo baadaye, inawezekana ukawa hukumbuki, lakini uchunguzi ukifanyika unafikishwa mahakamani bila kujua," alieeleza.




Tela la gari aina ya Scania lenye namba za usajili T639 DSW, lililokuwa limebeba shehena ya mizigo likiwa limeanguka kwenye mzunguko wa barabara ya Dodoma kuelekea Morogoro karibu na eneo la stendi ya mabasi ya Shabib, Makole jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Askofu Thadey ataja wagombea wenye sifa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la International Evangelism Sinai Mkoa wa Dodoma, Selvester Thadey, amewataka Watanzania katika kipindi hichi cha kuelekea uchaguzi mkuu 2020, kutowachagua wanasiasa wenye mihemuko ya kisiasa.

Pia amewaomba Watanzania kuhakikisha wanawachagua viongozi wenye sera zenye tija na watakaodumisha amani na mshikamo ndani ya nchi bila kujali itikadi yoyote ya kidini au kisiasa.

Thadey aliyasema hayo wakati akihitimisha maombi ya kuombea uchaguzi yaliyofanyika siku 21, katika kanisa hilo lenye makao yake Ipagala jijini Dodoma.

Alisema kuelekea uchaguzi huo Watanzania wanatakiwa kujihadhari na wanasiasa ambao watabainika kuwa na mihemuko, inayohatarisha amani na utulivu wa nchi uliopo.

"Sisi kama kanisa tumefanya maombi ya siku 21, kwa ajili ya kuliombea taifa na uchaguzi mkuu ili uchaguzi huo usiwe na mihemuko itakayoashiria kuwapo kwa vurugu, vitisho, matusi, ila ni imani yetu uchaguzi utakuwa wa amani, huru na uwazi," alisema Askofu Thadey.

Katika hatua nyingine, askofu huyo aliwaomba watumishi wa Mungu wawapo madhabahuni watumie nafasi zao kuhubiri amani na si kufanya siasa katika makanisa yao.

"Ila hapa pia nalazimika kusema kuwa hata hivyo kwa upande wa kanisa pia hazuiwi kiongozi yoyote wa kidini kuwa mwanasiasa isipokuwa achague moja asichanganye vitu viwili kwa pamoja kama tunavyoona kwa Askofu Gwajima kujitokeza kugombea, lakini tulikuwa na marehemu mama Lwakatare na kuna Mchungaji Msigwa," alisema.

Aidha, kwa upande wake Askofu Dk. Israel Gabliel Maasa kutoka Arusha, aliwataka wananchi kwenye kipindi hiki cha uchaguzi mkuu wawachague viongozi ambao watayaenzi mambo yaliyoachwa na viongozi wengine.

"Niwaambie tu ndugu zangu tuangalie na tuchague wale viongozi ambao wanajali watu, wanyonge na watakaotetea maslahi ya wananchi," alisema.

Aidha, Askofu Dk. Maasa alitoa wito kwa viongozi wote wa kiroho pindi wanapokuwa madhabahuni wasichanganye siasa na dini.

"Hili ni tatizo kubwa sana kiongozi wa dini hatakiwi kuchukua mambo ya siasa na kuyaleta katika madhabahu hili halifai," alisema askofu huyo.

Hata hivyo, alihamasisha jamii na waumini wote wa dini zote nchini waangalie na wachague viongozi ambao wana sera nzuri na si lugha za matusi.



# RC Mbeya awaonya mafundi simu za wizi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewataka mafundi simu katika mikoa ya Mbeya na Songwe kuwa makini na wateja wanaopeleka simu kujiridhisha kwanza kama si za wizi ili kutoingizwa kwenye mtego wa uhalifu.

Chalamila alitoa angalizo hilo jana wakati akifungua mafunzo ya wiki tano kwa mafundi simu wa mikoa hiyo ambayo yaliratibiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema wakati mwingine wahalifu huwaingiza mkenge mafundi simu kwa kuwapelekea simu aidha zilizotumika kwenye uhalifu au zilizoibwa na kusababisha mafundi hao kuingia kwenye matatizo.

**Ufundi ni sekta ambayo inatajwa kuwa na mchango mkubwa katika mabadiliko ya ukuaji wa uchumi utokanao na viwanda.**

Badala yake alisema wawe makini kwa kuhakikisha wanapewa stakabadhi au risiti za manunuzi ya simu hizo ili kujiepusha na mkono wa sheria.

"Siku hizi wezi wanawaingiza mkenge mafundi simu. Wanaiba simu huko halafu wanaenda kwa mafundi hao ama kuomba waziflashi au kutafutiwa wateja bila kujua, watu hao wanaingia mikononi mwa sheria. Kupitia mafunzo haya nawaomba mkawe makini msikubali kupokea pokea vitu msivyojiridhisha," alisema Chalamila.

Chalamila pia aliwahamasisha mafundi hao kuongeza ujuzi na maarifa ili kujiongezea kipato na kudhibiti vitendo vya wizi.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba, alisema mafunzo hayo yawahusisha vijana 100 na yanalenga kuwajengea uwezo mafundi simu nchini kote ili kufanya kazi zao kwa weledi na kuchangia pato la taifa.

Alisema mafunzo hayo yalianzishwa mwaka 2018 na yanalenga kuwapa maarifa mafundi simu namna ya kuongeza ujuzi wa kurasimisha ufundi wao na kuleta tija.

Mwenyekiti wa Umoja wa Mafundi Simu Mkoa wa Mbeya, Fredy Mnyalu, alishukuru kwa kupatiwa mafunzo hayo na kwamba watahakikisha wanashirikiana na serikali kufikia mapinduzi ya viwanda.

Alisema ufundi ni sekta ambayo inatajwa kuwa na mchango mkubwa katika mabadiliko ya ukuaji wa uchumi utokanao na viwanda.

Kwa mujibu wa Kilaba, hadi sasa takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania ina simu zinazofanya kazi milioni 48, lakini lengo ni kuwa na kiwanda cha kutengeneza simu za mikononi ifikapo mwaka 2021.



Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kupitia CCM, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akijadiliana jambo na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba, kabla ya kurejesha fomu ya kuwania nafasi hiyo kwa msimamizi wa uchaguzi, jijini humo, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wajane wajengewa nyumba za kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WAJANE sita wa Kata ya Mwaya wilayani Kyela, wamenufaika na msaada wa kuboreshewa makazi uliotolewa na Shirika lisilo kiserikali la Vision Trust Tanzania linalojishughulisha na huduma kwa yatima, wajane na wagane.

Akizungumza na Nipashe jana, mmoja wa wajane hao, Editha Makula (70), ambaye anaishi na wajukuu saba alioachiwa na watoto wake watatu ambao kwa sasa ni marehemu, alisema awali alikuwa anaishi kwenye nyumba ya udongo iliyoezekwa kwa nyasi na kwamba msimu wa mvua walishindwa kulala.

Makula alisema baada ya kuona mazingira anayoishi, Vision Trust iliamua kumjengea nyumba ya kisasa ili aondokane na adha aliyokuwa akiipata.

"Sikuwahi kuwaza kama nitakuja kuishi kwenye nyumba nzuri kama hii, maana sina uwezo wowote wa kifedha. Watoto wangu niliokuwa nawategemea wote walifariki (dunia) na kuniachia wajukuu saba ambao nawalea," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Mchungaji Clement Mwaitebele, alisema jumla ya Sh. milioni 40 zilitumika kwenye ujenzi wa nyumba sita ambazo zilijengwa katika Kata ya Mwaya.

Alisema walishawishika kuwajengea wajane hao nyumba baada ya kuona wakiishi kwenye nyumba zenye usalama mdogo. Alisema nyumba hizo zilikuwa zimejengwa kwa mianzi na kuezekwa kwa nyasi.

"Mwaka 2010 tulianza kuwajengea wajane nyumba bora za kuishi na tulikuwa tunajenga kwa awamu kadri pesa zinavyopatikana. Tuliona nyumba ni kipaumbele cha kwanza kwao kwa sababu ya hali duni waliyo nayo na kushindwa kuhudumia vyema watoto yatima," alisema Mchungaji Mwaitebele.

Alisema kwa sasa wameboresha makazi kwa wajane wa Kata ya Mwaya pekee, lakini uhitaji ni mkubwa, hivyo wana malengo ya kuhudumia wajane wa wilaya nzima ya Kyela.

Aliongeza kuwa watoto 300 ambao ni yatima katika Kata ya Mwaya wanaosoma shule za msingi na sekondari, wamepatiwa msaada wa sare, madaftari, viatu, mashuka na kupatiwa uji kila Jumamosi.

Mchungaji Mwaitebele alisema watoto hao walikuwa wanakosa mahitaji hayo muhimu kutokana na familia zao kuwa duni na kwamba wengi wanaishi kwa bibi zao.

Aliiomba serikali kuunga mkono juhudi hizo ili wajane na yatima waishi maisha ya furaha kama ilivyo kwa wengine na kwamba uhitaji bado ni mkubwa.

# Waomba masharti mikopo kuboreshwa

**Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKISHO la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Mbeya, limeomba serikali kuangalia upya masharti ya utoaji mkopo wa asilimia mbili kutoka halmashauri ili wanufaike na kumudu gharama za maisha.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLB) mkoani hapa, Joseph Mwandalima, wakati akizungumza na Nipashe serikali ilivyowawezesha kujikwamua na umaskini kupitia mikopo.

Alisema licha ya serikali kutoa fursa hiyo, bado kuna mlolongo mrefu wa kupata mikopo hiyo kutokana na masharti yaliyowekwa.

Mwandalima alisema masharti yaliyowekwa na halmashauri yamekuwa magumu kwao hali inayosababisha kukosa sifa ya kukopesheka, hivyo wanaiomba serikali kuangalia upya ni kwa namna gani watalisaidia kundi hilo.

"Miongoni mwa masharti ambayo halmashauri zetu zimeweka kwenye mikopo yao ni kwamba kila kikundi lazima kipate usajili na barua kutoka kwa watendaji wa vijiji. Sisi wenye ulemavu tumetawanyika, unashangaa wawili wako kijiji kimoja na wengine wako mbali. Sasa ni ngumu kuunganika kwa pamoja, hivyo cha muhimu watuhimize tujisajili bila kujali tunatoka kijiji kimoja," alisema Mwandalima.

Aliongeza kuwa licha ya vikwazo walivyonavyo aliwahamasisha wenzake kuendelea kuchapa kazi kwa kufanya shughuli ndogo ndogo za kujiingizia kipato.

Mwenyekiti wa SHIVYAWATA Mkoa, Luca Mahenge, aliomba serikali iangalie upya utaratibu wa utoaji mikopo kwa kundi hilo kwa kuhakikisha wanarekebisha baadhi ya sera na sheria ambazo zinamnyima haki mwenye ulemavu kukopesheka.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ulemavu (CHAWATA) Mkoa wa Mbeya, Jimmy Ambilikile, alisema msaada kwa sasa kundi hilo si tegemezi tena kwani wameanzisha shughuli ambazo zinawaongezea kipato, lakini hitaji lao ni mikopo yenye masharti nafuu kutoka kwenye taasisi za kifedha na halmashauri.





# Aagiza ukarabati majengo maabara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslim Hija, amewapa siku mbili makandarasi wa kampuni ya Badri East Africa kuhakikisha wanakamilisha matengenezo madogo ya majengo ya maabara za sayansi yaliopo Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Akizungumza jana alipofanya ziara ya kukagua majengo ya maabara hizo zinazojengwa chini ya mradi wa huduma za jamii (ZISP), alisema ubora wa maabara hizo ni kuondoa kasoro zote zilizojitokeza ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Dk. Idrisa alisema pamoja na wizara kuyakubali majengo hayo, lakini hawataweza kusaini fomu za makubaliano mpaka pale wayakapofanyia marekebisho kasoro zote zilizojitokeza.

Aidha, aliwapongeza makandarasi wa ujenzi huo kwa uvumilivu mkubwa waliouonyesha katika kipindi chote cha ujenzi pamoja na kuwapo sitofahamu ambazo zilikuwa na lengo la kuweka ubora wa majengo hayo.

Kwa upande wake, Mhandisi Khalid Uhadi kutoka kampuni ya Badri East Africa, aliahidi kuyafanyia kazi haraka iwezekanavyo matengenezo yaliopo ili kufanya makabidhiano hayo.

Jumla ya maabara nne za kisayansi zinazosimamiwa na kampuni ya Badri East Africa kati ya maabara saba za sayansi, zimekaguliwa zikiwamo za Kijini Matemwe, Mkwajuni, Mahonda na Mtoni Kigomeni.

**Pamoja na wizara kuyakubali majengo hayo, lakini hawataweza kusaini fomu za makubaliano mpaka pale wayakapofanyia marekebisho kasoro zote zilizojitokeza.**

# Mwinyi kuchukua fomu ya urais leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Mwinyi, kesho anatarajiwa kuchukua fomu Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC).

Akizungumza jana na waandishi wa habari Mjini Zanzibar, Katibu wa Siasa na Uenezi, Catherine Peter Nao, alisema baada ya zoezi la uchukuaji fomu kwa mgombea huyo atazungumza na wanachama wa CCM katika viwanja vya Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui.

Alisema kuwa mgombea huyo ataondokea ofisi kuu za CCM Kisiwandui kwenda ZEC Maisara kuchukua fomu, ambapo atasindikizwa na viongozi wachache wa CCM.

"Msafara wa mgombea hautakuwa na watu wengi kwa sababu hatutaki tusimamishe shughuli za kijamii, tunafanya hivyo ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao," alisema Catherine.

Aidha, alisema CCM Zanzibar na Tanzania Bara haina wasiwasi na ushindi kwa wagombea wao.

Alieleza kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli wamefanya kazi kubwa katika kutekeleza ilani ya CCM, hivyo wana matumaini makubwa ya ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Akizungumzia kuhusu uteuzi wa wagombea uwakilishi Zanzibar, alisema kuwa kamati ya maadili ya CCM itakutana leo kwa ajili ya kujadili majina ya wagombea na kufuatiwa na kikao cha kamati maalum kitakachofanyika kesho.

Alisema baada ya hapo Kamati Kuu ya CCM itakutana Agosti 30 mwaka huu kwa ajili ya kuteua wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa majimbo 50 ambao watapeperusha bendera katika uchaguzi mkuu.

Katibu huyo aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kufanya siasa za kistaarabu na kuacha kutumia lugha chafu katika majukwaa ya kampeni za uchaguzi.

**CCM Zanzibar na Tanzania Bara haina wasiwasi na ushindi kwa wagombea wao.**



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Zanzibar, Catherine Peter Nao, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) jana, kuhusu mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya chama hicho, Dk. Hussein Mwinyi, kuchukua fomu ya kuomba uteuzi katika Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) leo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Balozi Iddi aagiza utekelezaji mpango maalum

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameuagiza uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuangalia mpango maalum wa muda mrefu utakaozingatia mahitaji halisi ya maeneo ya kazi kwa ajili ya miradi yao ya maendeleo.

Alisema mpango huo endapo utazingatiwa katika hatua za awali mbali ya kusaidia kupunguza gharama za fidia kwa mali za wananchi, pia utatoa fursa kubwa zaidi kwa mamlaka hiyo kujipangia mipango.

Balozi Iddi alisema hayo juzi alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigunda uliopo Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao kwa sasa ndege ndogo zina uwezo wa kuruka na kutua.

Alisema yapo matukio kadhaa yanayoendelea kushuhudiwa katika jamii, ambapo serikali hulazimika kulipa fidia kutokana na miradi mbalimbali inayotekelezwa na taasisi za umma baada ya maeneo yanayoanzishwa miradi hiyo kuwa ni mali za wananchi.

Balozi Iddi aliutaka uongozi wa mamlaka hiyo kuhakikisha kazi hiyo wanaitekeleza katika kipindi hiki kabla ya baadhi ya watu kuanza kuvamia maeneo hayo baada ya kuanza kwa ujenzi wa uwanja huo.

Aidha, alipongeza uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa jitihada zao za kusimamia ujenzi wa uwanja huo na kuushauri ni vyema ujenzi huo ukaenda sambamba na kujengewa uzio utakaoepusha watu kuingia kiholela kwenye eneo hilo.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeridhia kujengwa kwa uwanja huo kutokana na mabadiliko makubwa ya mwenendo mzima wa shughuli za utalii, biashara na mawasiliano ya usafiri wa anga kati ya Zanzibar, mikoa ya Tanzania Bara na hata nchi jirani.

Balozi Iddi alisema kwamba watalii waliojipangia kufanya matembezi katika ukanda wa kaskazini mwa Kisiwa cha Unguja kutokana na uwapo wa uwanja huo, wanaweza kwenda moja kwa moja kwa kutumia ndege kutoka maeneo tofauti badala ya usafiri wa gari, ambao kwa sasa umezidi msongamano mkubwa.

"Kwa vile uwanja huo utakapomalizika, utakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege zitakazobeba abiria zaidi ya 70 utasaidia kupunguza pia msongamano katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume," alisema Balozi Iddi.

Aliushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kufikiria wazo lingine la kuangalia uwezekano wa kuwapo kwa kiwanja kingine cha ndege katika ukanda wa kusini mwa kisiwa cha Unguja kwa lengo la kuimarisha huduma za kiuchumi nchini.

Naye Msimamizi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigunda, Mhandisi George, alisema kazi zinazoendelea uwanjani hapo kwa sasa ni ukamilishaji wa uwekaji wa kifusi kwa tabaka la mwisho.

Alisema kwamba hatua ya utandikaji wa lami kwenye uwanja huo inatarajiwa kuanza Oktoba mwaka huu ukiwa na urefu wa kilomita mbili zitakazowezesha kutua au kuruka kwa ndege kubwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Said Iddi Ndombogani, alisema ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kigunda ni miongoni mwa miradi mikubwa inayotekelezwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafiriashaji Zanzibar katika mpango kazi wake.

Ndombogani alisema mradi huo utahitaji kuwa na eneo lenye ukubwa wa hekta 400 zitakazofanana na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro ambao utawezesha ndege kubwa kuruka au kutua.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**

**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**GENERATE MONEY AND JOBS**

- Learn Designing winning Project Proposals
- Access Donors.
- Establish NGO
- **0784 505108/0718 437371/ 0769 505108**


## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO.....5.....OF 2020**

**In the matter of the Estate of the late...LUCKY MAPANDA**

**BY 1...SEBIA MAPANDA**
**2....................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above- named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 15 day of September...2020

Dated at MOROGORO this.. **25...day of August ...2020**

RESIDENT MAGISTRATE

115872002

**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo mjini Tanga**

**Usimamizi wa mirathi 134 /2020**

**Ombi la 1.)Abdallah Ally Shehoza......**
**2.)Hamduni Ally Shehoza..................kuteuliwa**
**Msimamizi wa miradhi ya marehemu Ally Abdallah Shehoza.............................................**

**Kwa yeyote anaehusika....................................................**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na miradhi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/09/2020..........kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe......24/8/2020

MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NEEMA RICHARD MWASWALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI VITARA** yenye namba za usajili **T 960 BBP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi

**MBE/MBE/RB/611031/2020**

215871702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PETER FRANCIS MWALULILI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T. 859 DPT** aina ya **TOYOTA ALLEX.** Chassis namba **NZE1210312470.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi

**MBE/MBE/RB/611068/2020**

115871802

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO.66/2020**

**NURU LAITON MWALAH::::::::::::::::::::::::::::::MDAI**

**DHIDI YA**

**VERISI POUR ARUMASI:::::::::::::::MDAIWA WA KWANZA**
**NMB BANK PLC MBALIZI:::::::::::::::::::::::::MDAIWA WA PILI**
**ADILI AUCTION MART::::::::::::::::::::::::::MDAIWA WA TATU**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

**KWA:VERISI POUR ARUMASI (MDAIWA WA KWANZA)**

Fahamu ya kwamba Nuru Laiton Mwalah amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 26/08/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda,Mwenyekiti wa Baraza.
Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe18/07/2020.

**A.Mapunda**
**Mwenyekiti**
**18/07/2020.**

115871902

**UTHIBITISHO WA USIMAMIMIZI WA MIRATHI**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**

**MIRATHI NA. 57 YA 2020**

**Maombi ya Barua ya Usimamizi wa Mirathi ya Marehemu JUDITH KOKWIJUKA ALOYCE**

**NA**

**ROGATUS RWEHUMBIZA LWAMLEMA............ MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanadaiwa kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia Mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za Usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 11 mwezi 9 mwaka 2020.

Imewasilishwa leo hii IJUMAA, tarehe 21 Mwezi 8 mwaka 2020.

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YAWILAYA KINONDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 236/2020**

**Ombi la SIGFRID EDWARD NYALUSI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MATRIDA FUNGAROHO HONGOLE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 18/08/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

115871302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MAHAKAMA)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MENGWE**
**WILAYA YA ROMBO**

**SHAURI LA MADAI NA 33 LA 2020**

**PAMPHIL SATOR MASASHUA......................MDAI**
**NA**
**THOBIAS SIST MMANDA.................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai mtajwa hapo juu amefungua madai dhidi yako katiaka Mahakama hii,wewe mdaiwa mtajwa hapo juu popote ulipo unajulishwa kuwa ufike katika Mahakama hii tarehe 10/09/20 saa 2:30 (mbili na nusu )asubuhi ili kujibu madai dhidi yako.
Unaagizwa kufika na mashahidi pamoja na vielelezo unavyotaraji kutumia kwenye kujibu madai kama vipo .
Kama wewe mdaiwa hutoudhuria katika Mahakama hii kwa tarehe na saa tajwa hapo juu, kesi hii ya madai dhidi yako itasikilizwa kwa upande mmoja na kutolewa maamuzi ya upande mmoja dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 17/08/2020.

SAHIHI NA MUHURI
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MENGWE

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MENGWE - ROMBO

115871402


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie*

*0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# UREJESHAJI FOMU ZA UTEUZI WA WABUNGE



Naibu Waziri wa Maji ambaye ni mgombea ubunge Jimbo la Pangani, Jumaa Aweso (aliyeshikwa bega), akipongezwa na wanaCCM wenzake, baada ya kurudisha fomu za uteuzi, jimboni humo jana. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**



Mgombea ubunge Jimbo la Kisesa, Luhaga Mpina (kushoto), akihakiki nyaraka muhimu kabla ya kurejesha fomu ya kuomba kuteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kugombea jimbo hilo, jana. Wengine ni Katibu wa CCM Wilaya ya Meatu, Charles Mazuri (kulia) ni Mwenyekiti wa chama hicho wa wilaya hiyo, Juma Mwiburi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, akiwapungia mikono baadhi ya wananchi waliojitokeza kumsindikiza wakati wa kurudisha fomu ya kugombea ubunge wa Arusha Mjini, kwa msimamizi wa uchaguzi wa jijini hilo jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**




Wakereketwa na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jimbo la Masasi Mjini, wakimsindikiza mgombea ubunge wao, Geofrey Mwambe, kurejesha fomu za kuomba uteuzi wa kugombea nafasi hiyo katika ofisi ya msimamizi wa uchaguzi jimbo hilo, mkoani Mtwara jana. **PICHA: HAMISI NASRI**



Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati), akiongozana na wanachama wa CCM, wakiwasili kwenye ofisi za Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Tanga jana, kwa ajili ya kurejesha fomu za kugombea nafasi ya ubunge wa jimbo hilo. **PICHA BONIFACE GIDEON**



Mgombea ubunge Jimbo la Kawe, Halima Mdee akisindikizwa na wapambe wake kuingia katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi Manispaa ya Kinondoni, kurudisha fomu ya kugombea nafasi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# RONALDINHO AACHIWA HURU PARAGUAY

**ASUNCION,** Paraguay

NYOTA wa zamani wa Barcelona na Brazil, Ronaldinho ameachiwa kutoka Paraguay baada ya kutoruhusiwa kutoka ndani kwa takribani miezi mitano.

Ronaldinho na kaka yake, Roberto Assis, walifungwa Machi mwaka huu baada ya kuingia nchini humo kwa kutumia hati za kusafiria za kughushi.

Wawili hao baadaye Aprili walitolewa jela ambako walikaa kwa muda wa siku 32 na kuhifadhiwa katika hoteli moja kwa amri ya kutotoka nje.

Ronaldinho, ambaye alikuwa nguzo katika kikosi cha Brazil kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 2002, na kaka yake waliachiwa juzi, Jumatatu.

Wakati Ronaldinho akitakiwa kulipa faini ya dola 90,000, kaka yake alipigwa faini ya dola 110,000.

Nyota huyo wa zamani wa klabu za Barcelona, Paris Saint-Germain na AC Milan alicheza mechi 97 kwa timu ya Taifa ya Brazil kati ya mwaka 1999 na 2013, akifunga mabao 33.

Ronaldinho pia alishinda tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2005.




# Arthur aaga kwa huzuni Barca

**BARCELONA,** Hispania

ARTHUR amesema ameonyesha hisia ya majonzi wakati akiaga Barcelona katika video aliyoiweka kwenye mtandao wa kijamii Jumatatu wakati akijiandaa kujiunga na Juventus.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil, Arthur alijiunga na Barca mwaka 2018 na alikuwa na mwanzo mazuri, huku akionyesha uwezo mkubwa wa pasi na akaanza kulinganishwa na gwiji, Xavi.

Lakini msimu wa 2019-20, alishindwa kujiimarisha yeye mwenyewe na kujikuta akikosa nafasi kwa kikosi hicho cha 'Blaugrana'.

Uvumi kuhusu majaliwa yake ulianza kuvuma wakati Ligi ya Hispania, LaLiga, ilipokumbwa na virusi vya corona, ingawa nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, alisisitiza hana mpango wa kuondoka baada ya kuhusishwa na Juve.

Lakini Juni stori hiyo ilithibitishwa kwamba, Arthur atajiunga na Juve kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 82, huku Miralem Pjanic akienda Camp Nou kwa euro milioni 65.

Na sasa wakati akijiandaa kwenda kujiunga na Juve, Arthur ameonyesha huzuni yake ya kuondoka Barcelona.

"Kusema kwa heri mara zote ni kitu kigumu, naondoka sehemu ambayo niliona kama nyumbani kwangu," alisema katika video aliyoiposti kwenye mtandao.

# Lewandowski anastahili Ballon d'Or - Gomes

**LISBON,** Ureno

ROBERT Lewandowski alistahili Ballon d'Or kama tuzo hiyo ikitolewa mwaka huu wa 2020, straika wa zamani wa Ureno, Nuno Gomes amesema.

Lewandowski alifunga mabao 55 katika mashindano yote msimu huu, yakiwamo 15 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kuiwezesha Bayern kutwaa mataji matatu, Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Tuzo ya Ballon d'Or imefutwa mwaka huu kutokana na msimu kuathiriwa na mlipuko wa virusi vya corona.

Gomes anaamini maamuzi ya kufuta tuzo hiyo si haki kwa Lewandowski, ambaye alitumia saa 24 kusherehekea ushindi wa Bayern wa 1-0 dhidi ya Paris Saint-Germain kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nafikiri anastahili kushinda Ballon d'Or kama tuzo hii ingekuwapo," alisema Gomes, akinukuliwa na Stats Perform News.

"Ni straika wa maangamizi kama unacheza dhidi yake. Unatakiwa jicho lako liwe kwake kwa sababu ukimpa nafasi kidogo tu atakufunga.

"Mmoja wa washambuliaji bora kwa sasa, hilo kwa uhakika kabisa."



HABARI MICHEZO

# Man City kusajili zaidi - Khaldoon

**MANCHESTER,** England

MWENYEKITI wa Manchester City, Khaldoon Al Mubarak amethibitisha kwamba klabu inapanga kuleta wachezaji zaidi wapya kwa ajili ya kuimarisha kikosi ili kuchukua Kombe la Ligi Kuu kutoka kwa Liverpool.

Kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola kilishindwa kurudia makali yake ya kutwaa mataji matatu msimu wa 2019-20, kikipitwa pointi 18 na Liverpool ambao walilibeba taji hilo.

Winga Ferran Torres na mlinzi Nathan Ake tayari wamewasili hapo kwenye dimba la Etihad kutoka Valencia na Bournemouth, kwa jumla ya ada ya pauni milioni 60.

Akizungumza na tovuti ya klabu hiyo, Khaldoon amesema City wanataka kuimarisha zaidi kikosi chao na watasajili wachezaji wengi kadri Guardiola atakavyohitaji.

"Tayari tumewasajili Ake na Ferran Torres, lakini tunataka kufanya usajili zaidi," alisema.

"Malengo yetu ni kuwa na kikosi kipana zaidi kwa msimu ujao, na kubwa ni kuhakikisha tunabeba mataji makubwa.

Msimu huu haukuwa mzuri sana kwetu, lakini tunajipanga kwa ajili ya msimu mwingine unaokuja.






# CHELSEA MAMBO BADO MAGUMU KWA HAVERTZ

**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Bayern Leverkusen, Rudi Voller amekanusha ripoti zinazodai wanakaribia kufikia makubaliano na Chelsea kumsajili Kai Havertz na kuziita "upuuzi".

Chelsea kwa miezi kadhaa imekuwa ikihusishwa sana na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Havertz mwenye umri wa miaka 21, wakati klabu hiyo ya Ligi Kuu ikiangalia namna ya kuboresha kikosi chake msimu ujao.

Vyombo vya habari Jumatatu vilidai kwamba klabu hizo mbili zinakaribia kufikia makubaliano ya usajili wa nyota huyo wenye thamani ya euro milioni 80.

Lakini Voller hana habari na taarifa hizo, akisema kuwa mpango huo bado uko mbali sana.

"Huu ni upuuzi," alisema akinukuliwa na gazeti la Sport Bild.

Kama Havertz atajiunga na Chelsea, ataungana na Hakim Ziyech na mchezaji mwenzake wa timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner.

Chelsea walishindwa kufanya usajili wa wachezaji wakati wa dirisha la msimu wa 2019-20 kutokana na kutumikia adhabu ya kutosajili baada ya kuvunja sheria ya kusajili wachezaji wenye umri mdogo.

# *Son ajipa changamoto ya kufunga Tottenham*

**LONDON,** England

NYOTA wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min amejipa changamoto yeye mwenyewe ya kunoa makali yake mbele ya goli msimu ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anaingia kwenye msimu wake wa sita Ligi Kuu ya England na alikuwa na kiwango bora zaidi kwa misimu minne iliyopita.

Mabao yake 14 kwenye Ligi Kuu msimu 2016-17, yamebakia kuwa rekodi kubwa zaidi kwake, baada ya kufuatia na mabao 12, kisha 12 tena na msimu wa 2019-20 kutikisa nyavu mara 11.

"Kwa kiasi fulani nina hasira juu yangu kwa sababu nimekosa nafasi nyingi za kufunga," alisema Son akinukuliwa na tovuti ya klabu yake.

"Msimu huu nataka kuwa na makali zaidi kwenye goli kuliko msimu uliopita. Kwani nataka kufunga na kufunga kila nikipata nafasi. "Najiimarisha mwenyewe ili niweze kufunga zaidi, na naamini nitarudi katika uwezo wangu wa kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja.

Spurs itaanza kampeni ya Ligi Kuu ya England nyumbani kwa Everton Septemba 12.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RAIS AFICHUA SIRI YA INTER, MESSI MEZANI

Si jambo rahisi kiuchumi, hilo liko wazi kabisa, lakini kikwazo kikubwa ni nia ya yeye...

**MILAN,** Italia

INTER Milan pengine tayari imeshaanza mazungumzo ya kuwania kumsajili Lionel Messi kutoka Barcelona, Rais wa zamani wa klabu hiyo, Massimo Moratti amesema.

**Nerazzurri wamekuwa wakitajwa kama moja ya klabu inayojaribu kumsajili nyota huyo wa Argentina kama akichagua kuondoka pale Camp Nou.**

Messi amedaiwa kwamba anafikiria zaidi kuhusu majaliwa yake baada ya kuwa na msimu mbaya ukimalizwa kwa kichapo cha fedheha cha mabao 8-2 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kutoka Bayern Munich.

Moratti, Rais wa Inter kati ya mwaka 1995 na 2013, anafikiri tangazo la hivi karibuni kwenye televisheni ya wamiliki wa sasa wa klabu hiyo, Kampuni ya Suning group - ikionyesha kwamba wana mradi mpya utakaofanya mabadiliko makubwa kwenye timu hiyo, unaonyesha kwamba, Messi anaweza kutua hapo kwenye dimba la San Siro.

"Si jambo rahisi kiuchumi, hilo liko wazi kabisa. Lakini kikwazo kikubwa ni nia ya Messi mwenyewe," alisema Moratti akiiambia AS.

"Unatakiwa uelewa kwa hakika kabisa kama anataka kuondoka Barca. Sina uhakika na hilo kabisa.

"Fikiria Inter tayari wamejaribu kumsajili yeye. Hata kama tangazo hilo la Suning halihusiani na nyota huyo wa Argentina, lakini hilo linanifanya nifikiri kwamba tayari mazungumzo yamefanyika.

"Kama sivyo, watafanya hivyo hivi karibuni."

Inter kwa sasa haina upungufu kwenye safu ya ushambuliaji, kwani Romelu Lukaku na Lautaro Martinez kwa pamoja wametikisa nyavu mara 55 katika mashindano yote msimu wa 2019-20.

Moratti amekuwa anavutiwa zaidi na uharaka wa Lukaku kuzoea soka la Italia tangu alipotua hapo akitokea Manchester United mwaka jana.

## ZISIKUPITE

### BARCA, SUAREZ KUACHANA

BARCELONA watasitisha mkataba wa straika wao, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 33 raia wa Uruguay. ***(RAC1, via Mail)***

### ARTETA KUMRESHA BERGKAMP

KOCHA Mikel Arteta anataka gwiji wa zamani wa Arsenal na Uholanzi, Dennis Bergkamp kurudi klabuni hapo kama kocha msaidizi. ***(Sun)***

### CHELSEA KUTISHA SOKONI

CHELSEA wanaweza kutumia fedha nyingi zaidi kuliko dirisha la usajili lililopita baada ya kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21, kutoka Bayer Leverkusen na mlinzi wa Paris St-Germain na Brazil, Thiago Silva, 35. ***(Times)***

### BELLERIN AWANIWA PSG

MLINZI wa kulia wa Arsenal na Hispania, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 25, amepewa ofa na Paris St-Germain. ***(Times)***

### CITY KUTUMA OFA KWA MESSI

MANCHESTER City wanajaribu kuangalia kama wanaweza kutuma ofa Barcelona kwa ajili ya kumsajili Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, endapo akitaka kuondoka kule. ***(ESPN)***

### DE BEEK ASIKILIZIA KLABU EPL

KIUNGO wa Ajax na Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 23, anasubiria ofa kutoka klabu za Ligi Kuu ya England. ***(Sky Sports)***

### SARR KUTUA CHELSEA

CHELSEA pia wanaweza kumsajili mchezaji wa Ufaransa, Malang Sarr ambaye yupo huru kwa sasa, ikimtaka kwa mkataba wa miaka minne. Mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 21, aliondoka pale Nice kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Telefoot, via Mail)***

### YAJITOSA KWA ALLAN

EVERTON imefikia makubaliano na Napoli kulipa pauni milioni 31.5 kwa ajili ya kumsajili kiungo, Allan mwenye umri wa miaka 29, raia wa Brazil. ***(Express)***

### LINDELOF AWASHUKURU POLISI

MLINZI WA Manchester United, Victor Lindelof mwenye umri wa miaka 26, amewashukuru polisi wa Sweden kwa kumkamata mwizi aliyemkaba mwanamke mzee. ***(Sky Sports)***

### WOLVES KWA MAITLAND-NILES

KLABU ya Wolves ipo kwenye mazungumzo na Arsenal kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa pembeni, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 22. ***(Sky Sports)***

### LEEDS YAMFUATA GONZALEZ

LEEDS United inawania kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Nicolas Gonzalez mwenye umri wa miaka 22, amesema Mkurugenzi wa Michezo wa Stuttgart, Sven Mislintat, klabu ambayo nyota huyo anaichezea kwa sasa. ***(Yorkshire Evening Post)***

## HABARI MICHEZO

### Azam yafunga na Mcameroon

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC imetangaza rasmi kuwa imefunga usajili kwa msimu wa 2020/21 kwa kuwasajili wachezaji wawili, Allain Thierry Akono kutoka Cameroon, huku ikimwongeza mkataba wa mwaka mmoja, nahodha wa klabu hiyo, Aggrey Morris.

Kama vile haitoshi, klabu hiyo imefunga mjadala wa mchezaji Salum Aboubakar na kusema kuwa ataendelea kubaki hapo kwa msimu unaoanza Septemba 6, mwaka huu.

Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema juzi kuwa kuanzia siku hiyo anatangaza kuwa wamemaliza rasmi usajili na wamefunga kila kitu, wanachosubiri sasa ni Ligi Kuu na michuano mingine inayokuja mbele yao ianze.

Akono amesajiliwa kama mchezaji huru akitokea klabu ya Fortuna du Mfou ya nchini humo.

### Ligi Kuu Wanawake Z'bar kuanza Sept. 6

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Wanawake Zanzibar, inatarajiwa kuanza kutimua vumbi mapema Septemba 6 kwa msimu wa 2019/2020 kabla ya kumalizika Septemba 23, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Wanawake Zanzibar, Nasra Juma, alisema ligi hiyo itashirikisha jumla ya timu tano za wanawake ambazo ndizo zipo visiwani hapa kwa sasa.

Alizitaja timu hizo ni Women fighter, Green Gueens, New Generation, Jumbi Queens na Kidimni Queens zote kutoka Unguja na kwamba kamati hiyo inaendelea na jitihada zake ili kupata timu za mpira wa miguu kwa upande wa Pemba.

Alisema ligi hiyo inatarajiwa kuchezwa katika Uwanja wa Mau B pekee majira ya saa 10:00 alasiri na amewataka wadau wa soka kujitokeza kwa wingi ili kuweza kuzipa hamasa timu hizo.

"Tunacheza ligi tukiwa na timu tano za wanawake ambazo zote ni kutoka Unguja, lakini kamati inaendelea kuwasiliana na timu moja ambayo ilikuwa kisiwani Pemba ili kuona msimu wa ujao wa 2020/21 inacheza ligi. Tunaamini ligi itakayochezwa pengine inaweza kuwa chachu ya mafanikio ya kupata timu nyingi," alisema.

# FRAGA ARUDI KWAO BRAZIL, SVEN AANIKA SABABU

**Na Saada Akida**

KIUNGO mkata umeme wa Simba, Gerson Fraga, amewashtua mashabiki wa klabu hiyo baada ya kuondoka nchini ghafla na kurejea kwao Brazil wakati huu Simba ikitarajiwa kushuka Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha Jumapili kuivaa Namungo FC kwenye mechi ya Ngao ya Jamii.

Nipashe lilipomtafuta Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, jana kujua kulikoni kiungo huyo amendoka, alisema ni kweli Fraga amelazimika kuondoka baada ya kupewa taarifa kwamba anatakiwa nyumbani kwa sababu ya matatizo ya kifamilia.

**Alisema atalazimika kumkosa nyota huyo kwa muda mfupi kabla ya kurejea nchini kuendelea na majukumu yake, kwa sababu ni miongoni mwa wachezaji walikuwapo katika programu zake kwa msimu mpya wa 2020/21.**

"Fraga amepata ruhusa maalum na ameenda kwao kuweka sawa matatizo ya familia yake, baada ya kumaliza atarejea mapema na kuungana na wenzake katika kuendelea na majukumu yake ya kazi," alisema Sven.

Alisema anatarajia ndani ya wiki hii kikosi chake kitakamilika baada ya beki Pascal Wawa kutua nchini leo akitokea nchini kwao baada ya ruhusa maalum.

Kwa upande wa Fraga, amewaondoa hofu mashabiki wa Simba akisema ameondoka kwa ajili ya matatizo ya kifamilia pekee na atatejea mapema kuendelea na majukumu yake ya kazi.

"Mashabiki wanatakiwa kupotezea mitandao ya kijamii hasa kuhusu barua ambayo ilikuwa ikisambaa, mimi bado nipo Simba kwa mujibu wa mkataba wangu," alisema Fraga.

Nyota huyo alikuwapo katika tamasha la Simba Day na kikosi cha 'Wekundu wa Msimbazi' na alicheza kipindi cha pili kama beki wa kati wakati wakishinda 6-0 kwenye mechi ya kirafiki iliyopigwa Uwanja wa Mkapa dhidi ya Vital'O ya Burundi.




Balozi wa kinywaji cha Sayona Twist, Rajab Abdul Kahali maarufu Harmonize (aliyesuka nywele), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mwonekano wa lebo mpya ya Sayona Twist ambayo ina picha yake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Harmonize afunguka sura yake chapa ya Sayona*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI sura yake ikianza kuonekana kwa mara ya kwanza katika mwonekano mpya wa lebo ya chapa ya Sayona Twist, balozi wa kinywaji hicho, Rajab Abdul Kahali maarufu kama Harmonize, ameahidi kutumia ubalozi wake huo kuhakikisha Sayona inakuwa chaguo namba moja sokoni.

Harmonize alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam, wakati kampuni ya utengenezaji wa vinywaji baridi inayokua kwa kasi Tanzania, Sayona Drinks Limited, ikizindua rasmi mwonekano mpya wa lebo ya chapa yake ya Sayona Twist katika juhudi za kuwafikia wateja wengi zaidi na kuleta utofauti sokoni.

Harmonize 'Konde Boy', alisema amejisikia fahari kufanya kazi na kampuni ambayo ni ya ubunifu iliyojikita katika kuwaridhisha wateja wake kila wakati.

"Mtazamo wa aina hii, unaenda sambamba na maono ambayo sisi huko 'Kondegang' tunayo. Kwa upande wangu, nitaendelea kusaidia Sayona Tanzania kuwafikia Watanzania wengi zaidi ili kuhakikisha Sayona Twist inaendelea kuwa chaguo namba moja sokoni," alisema.

Kwa upande wa mmoja wa wakurugenzi kutoka Motisun Group ambao ndio wamiliki wa Kampuni ya Sayona, Veer Patel alisema mwonekano mpya wa lebo hizo umechochewa na lebo asili za chapa hiyo, huku lebo mpya zikiwa ni za kisasa zaidi na ubora ambazo zimeambatana na picha ya balozi wao, Harmonize.

Patel alisema uzinduzi wa lebo hizo mpya ni hatua muhimu katika safari ya chapa hiyo, ikiwa ni chapa ya kwanza ya nyumbani kuunga mkono kipaji cha msanii wa hapa nchini katika kuzipeleka chapa za ndani kimataifa.

Alisema historia nzuri ya chapa ya Sayona Twist ni ile iliyojaa uvumbuzi na uridhishaji wa hali ya juu wa mteja, kati ya mambo ambayo yanaifanya kuwa moja ya chapa inayokua kwa kasi katika soko la Tanzania.


Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Mauzo wa Sayona Tanzania, Emmanuel Laswai, alisema, sura mpya ya chapa ya Sayona Twist itapatikana katika ladha na bidhaa zote za chapa Twist.

"Mwonekano mpya wa lebo za chapa ya Sayona Twist unakamilisha upekee wa kinywaji cha Sayona Twist, kuhakikisha kuwa chapa hiyo inaendelea kuwa kipenzi cha Watanzania," alisema Laswai.

Michezo

Jumatano Agosti 26, 2020

Nipashe



Rais afichua siri ya Inter, Messi mezani UKURASA 22

AMETUA...




Msafara wa mashabiki wa Yanga wakiongozana na gari iliyombeba kiungo mpya wa klabu hiyo, Carlos Fernandes 'Carlinhos', baada ya kumpokea jana katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, akitokea Angola tayari kujiunga na kikosi cha timu hiyo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## ...Yalia kubanwa kibali cha Morrison

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga imeeleza kushangazwa na namna inavyokomaliwa na serikali kurejesha wizarani kibali cha kufanya kazi cha kiungo aliyejiunga na Simba, Mghana Bernard Morrison.

Akizungumzia suala hilo jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema walipokea barua kutoka kwa ofisa mmoja wa wizara ya kazi ikiwata kurejesha kibali cha Morrison cha kufanya kazi nchini, lakini wakawajibu kuwa bado ni mchezaji wao.

"Tunashangaa kwa nini watuambie turudishe kibali chake haraka, kwa nini katika suala hili waliingilie kwa kiasi hiki, hatujawahi kuona wizara ikifanya hivi katika kipindi chote. Tumewajibu bado ni mchezaji wetu maana bado ana mkataba na sisi," alisema.

Lakini alipoulizwa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Crescentius Magori endapo klabu hiyo imetia mkono katika suala hilo wizarani, alisema kwa mujibu wa taratibu kawaida unapoomba kibali cha kazi lazima wizara iombe kile cha awali kama mfanyakazi husika alishafanya kazi nchini katika taasisi yoyote.

Magori, alifafanua kuwa Simba ilichokifanya ni kufuata taratibu kwa kuomba kibali na kwamba hata kama Yanga wakikataa kukirejesha, wizara yenye mamlaka inaweza kutoa kingine kwa kueleza cha awali kimepotea.

"Kwanza kwa utaratibu ukiomba kibali cha mchezaji lazima upitie TFF (Shirikisho la Soka nchini) na baada ya hapo ikishapitisha, ndipo uende wizarani, na suala hili lilivyo tayari TFF ilishatangaza Morrison ni mchezaji huru, hivyo kwa Simba hilo halina tatizo," alisema.

# Carlinhos aahidi mazito Yanga

**Na Saada Akida**

## Asema hakutegemea kupokewa na umati wa mashabiki akipitishiwa Msimbazi, gari Simba lazuiwa...

HUKU akishangazwa na umati wa mashabiki wa Yanga waliojitokeza Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kumpokea, kiungo anayeelezwa ni fundi wa kucheza eneo la ukabaji na ushambuliaji, Carlos Stenio Fernandes Guimaraes 'Carlinhos', amesema kazi yake ni moja tu, kuhakikisha klabu hiyo inafikia malengo yake.

**Umati mkubwa wa mashabiki wa Yanga walijitokeza jana kumpokea Carlinhos, aliyejiunga na timu hiyo akitokea Klabu ya G.D. Interclube ya Angola, na kusindikiza msafara wake kutoka Julius Nyerere hadi makao makuu ya Yanga, mtaa wa Twiga na Jangwani wakipitia Msimbazi yalipo makao makuu ya watani zao, Simba.**

Akizungumza kwa kifupi baada ya kutua, Carlinhos alisema anafurahi kujiunga na Yanga na anaamini atapambana kufikia malengo ya timu hiyo.

Nyota huyo ambaye alitua na ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia majira ya saa 7:20 mchana na kupokewa kwa shangwe kubwa, alisema amefurahi kupokewa na umati mkubwa wa mashabiki.

"Nimefurahi kuona mapokezi makubwa ya mashabiki, lakini kuja kuichezea timu ya Yanga na kuhakikisha tunafikia malengo yanayotarajiwa," alisema Carlinhos.

Carlinhos ambaye ni wa Angola, amemalizana na Yanga kwa dili la miaka miwili, hivyo atakuwa miongoni mwa nyota watakaotambulishwa rasmi Jumapili Agosti 30 kwenye kilele cha Wiki ya Wananchi katika Uwanja wa Mkapa.

Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, Mhandisi Hersi Saidi, ambao ni wadahamini wa Klabu ya Yanga, waliofanikisha usajili huo, alisema nyota huyo amewasili nchini na ni mchezaji halali wa Yanga kuanzia sasa.

"Tayari mchezaji amewasili, sasa ni mali halali ya Yanga, yupo tayari kuitumikia timu yetu kwa kipindi ambacho tumekubaliana," alisema Hersi.

Carlinhos anaungana na wachezaji wengine wapya watatu ambao tayari wametia saini msimu huu kujiunga na kikosi cha Yanga, ambao ni Mghana Michael Sarpong na Wakongomani wawili, Tuisila Kisinda pamoja na Mukoko Tunombe.

Hata hivyo, kesho Yanga inatarajia kumpokea straika mwingine raia wa Burkina Faso, Sogne Yacouba aliyekuwa akiichezea Asante Kotoko ya Ghana, tayari kwa ajili ya kujiunga na timu hiyo wakati huu ikitarajia kuwatambulisha rasmi Jumapili Agosti 10 kwenye kilele cha Siku ya Mwananchi.

Katika mapokezi hayo ya Carlinhos jana, mashabiki wa Yanga walivania gari ndogo ya Simba aina ya Hiace ambayo ilifika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere kumpeleka mshambuliaji wao, Chris Mugalu, aliyekuwa akisafiri kuelekea kwao DR Congo.

Polisi waliokuwapo uwanjani hapo walilazimika kuwatawanya mashabiki hao na kulizuia gari hilo la Simba kwa zaidi ya saa moja na nusu hadi walipohakikisha msafara wa mashabiki wa Yanga umeondoka na kufika mbali.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Habari na Hamasa kuelekea kilele cha Siku ya Mwananchi, Suma Mwaikenda, alisema maandalizi ya kilele hicho yanaenda vizuri na tiketi zitaanza kuuzwa leo kwa kiwango cha Sh. 5,000 mzunguko, VIP A Sh. 30,000, huku VIP B na C zikiuzwa kwa Sh. 20,000 na kwa watu maalum Sh. 200,000.

Katika kilele hicho, Yanga itacheza mechi ya kirafiki dhidi ya mabingwa wa Burundi, Aigle Noir.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002